Nipashe

Ijumaa Februari 5, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580482

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




**MAGEREZA** yapewa rungu kwa wadaiwa sugu mabilioni yake

UKURASA 3



**SPIKA** alia wabunge wengi hawajampa taarifa za umri wao

UKURASA 2

UKURASA 11

# JPM: Dawa hizi ndizo zinatufaa



UKURASA 2



Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Zena Ahmed Said, akifafanua jambo katika mahojiano na waandishi wa habari wa kampuni ya The Guardian Ltd, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

MAHOJIANO MAALUM

# Mahakama Maalum ya Ukatili inakuja

UKURASA 4

UKURASA WA 5

## WANANE KORTINI TUHUMA UNYANG'ANYI KWA SILAHA

WATU wanane wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita kwa kosa la unyang'anyi wa kutumia silaha kwa kuvamia kituo cha mafuta Mara...

UKURASA WA 7

## KANISA LASISITIZA HADHARI MAGONJWA YA MLIPUKO

KANISA la Anglikana Mkoa wa Lindi, limewashauri waumani wake kuchukua tahadhari kwa kunawa mikono kwa maji tiririka, kabla na baada ya kuingia ndani ya kanisa na kukaa kwa nafasi...

## MCHUNGAJI AZUIA WATOTO KUSOMA

UKURASA 5

**MICHEZO** MASHABIKI YANGA WAMSUBIRI FISTON UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

HABARI KITAIFA

# Serikali yapata dawa migogoro ya ardhi wananchi na hifadhi

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia upya ramani za mipaka ya Hifadhi za Taifa na Mapori Tengefu ili kumaliza mkanganyiko na kuondoa migogoro kati yake na wananchi.

Vilevile, ameagiza wizara hiyo kuanzisha kambi ndogo za vikosi vya askari wa wanyamapori katika maeneo yote yanayokabiliwa na tatizo la uvamizi wa wanyamapori kama tembo ili wananchi wasisumbuliwe.

Aliagiza kufanyika kwa mapitio hayo jana, wakati akijibu swali aliloulizwa na Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Kenani, katika kipindi cha maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu.

Katika swali lake la msingi, Kenani, alitaka kujua serikali ina mkakati gani wa haraka wa kwenda kupitia upya maeneo ambayo yanasababisha migogoro na wananchi ili mipaka hiyo ieleweke.

"Mheshimiwa Waziri Mkuu, dhana ya kutenga maeneo na kusimamia hifadhi zilizopo nchini ni shirikishi. Sote tunajua wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi mbalimbali ni wahifadhi namba moja, jambo ambalo kwa sasa limebadilika kulingana na watendaji, aidha wachache au kulingana na mambo yanayofanyika hivi sasa.

"Natambua kumekuwa na kelele nyingi na malalamiko mengi kutoka kwa sisi wabunge kwa wananchi wetu. Leo wananchi wanaozunguka hifadhi ambao wanashughulika na shughuli kama za kilimo, ufugaji na uvuvi wamekuwa wakipigwa, kunyanyaswa na kunyang'anywa mifugo, jambo ambalo linakwenda kuondoa dhana ya wao kuwa wasimamizi wa hizi hifadhi," alisema.

Alisema miongoni mwa matatizo yanayosababisha vurugu hizo ni mipaka inayobadilishwa kila siku na mipaka mingine ambayo haijawekwa vitu ambavyo vinaonyesha alama kuwa hapa ni mpaka.

Akijibu swali hilo, Waziri Mkuu alisema migogoro hiyo mara nyingi imetokana na kutoeleweka kwa uwepo wa mipaka kama ambavyo Mbunge alivyosema.

# JPM: Dawa hizi zinatufaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli amewataka Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona, akibainisha kuwa baadhi ya dawa ikiwamo Covidol, zimethitishwa kuua bakteria na virusi kwa asilimia 99.9.

Akizungumza jana kwenye uzinduzi wa Makao Makuu ya Jeshi la Magereza huko Msalato jijini hapa, Rais Magufuli alisema kuna dawa nyingi ambazo ni nzuri zilizothibitishwa na Mkemia Mkuu wa Serikali kufanya kazi vizuri ya kuua bakteria na virusi.

"Sisi Tanzania tumeshashinda, mbele za Mungu hakuna kitakachoshindikana, tuendelee kuchukua tahadhari, lakini kuna dawa nyingi tu ambazo ni nzuri za kujifukizia kama mnavyoshauriwa.

"Kuna dawa inaitwa Covidol, Bupiji zile zinafanya kazi kwa sababu zimethibitishwa na Mkemia Mkuu," alisema.

Aliwataka Watanzania wajitambue na wasikubali kutumika kwenye biashara za wengine. "Nimeshatoa wito kwa taasisi zinazosimamia dawa za asili ziziendeleze, dawa hizi za asili zilipigwa vita na wakoloni kwa sababu ya uchumi. Ukiwa na mti wako, hata kama unaponya malaria, utaambiwa huu ni mti wa kishamba.

"Sisi tulikubali kwa sababu tuliona wao wanajua kila kitu, Mungu ametupa mimea na tukabarikiwa, tuitumie.

"Kwa hiyo, Wizara ya Afya inayosimamia dawa za asili, huu ni wakati wa kutumia kikamilifu, ninarudia kutoa wito kwa Wizara ya Afya isiwakatishe tamaa wataalamu hawa wapo, wengine madaktari, kuna mtu anaitwa Profesa Malebo, amevumbua dawa inaitwa Covidol," alisema.

Alibainisha kuwa hata madaktari wanatumia dawa hizo kujifukizia.

"Wakija huku wanawatwanga sindano, huu ndiyo ukweli. NIMR wamegundua dawa inatumika, tushikamane ndugu zangu, tutashinda kila jambo kwa sababu Mungu wetu yupo pamoja na sisi," alisema.

Kuhusu mbegu za GMO, alisema hatua ya jeshi hilo kuzalisha mbegu za mazao mbalimbali ikiwamo mchikichi, ni nzuri kwa kuwa inasaidia kulinda mbegu zilizopo nchini na si za kutoka nje ya nchi.

"Sh. bilioni 443 hadi 470 zinatumika kwa mwaka kuagiza mafuta, tutahakikisha tunawawezesha kukamilisha miradi ya kimkakati, hizo Sh. bilioni 13 zilizokuwa zimepangwa kujenga Makao Makuu ya Magereza, ombi la kubadilisha matumizi ya kutekeleza miradi ya maendeleo ninakubaliana na ninyi," alisema.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, akitoa maelezo kwa waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu gari aina ya Landrover, lililoko ofisi za Makao Makuu ya chama hicho, lililotumiwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere katika harakati za kudai uhuru, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 44 ya kuzaliwa CCM. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Spika alia wabunge wengi kutompa taarifa umri wao

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amepiga marufuku wabunge kutumia nembo ya Bunge katika nyaraka zao binafsi, kwa kuwa kufanya hivyo ni kosa la jinai.

Wakati akisitisha shughuli za Bunge jana mchana, Spika Ndugai alisema kuwa kwa mujibu wa sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge, nembo ya Bunge inatumika katika nyaraka za Spika au watendaji wa Bunge hilo tu.

Kutokana na matumizi mabaya ya nembo hiyo, alisema yeyote asiyebainika kuitumia wakiwamo wabunge, watakuwa wamefanya kosa la jinai.

Akionyesha kutofurahishwa na matumizi yasiyo sahihi ya nembo hiyo, Spika Ndugai alisema tayari alishatoa katazo kwa wabunge kutotumia nembo hiyo, lakini mbaya baadhi yao wameendelea kuitumia katika nyaraka zao binafsi.

"Kuna wabunge wameendelea kutumia nembo hii katika nyaraka zao binafsi za kuteua wasaidizi wao au kuwafukuza. Yupo mbunge mmoja jana (hakumtaja), aliandika barua yake binafsi ya kutangaza nafasi za ufadhili kwa masomo ya shahada ya uzamili na shahada ya kwanza," alisema.

Spika Ndugai alifafanua kuwa mbunge huyo alitumia nembo hiyo kwenye barua yake binafsi, huku akijua Bunge halihusiki wala kujua suala hilo.

"Matumizi halali ya nembo ni barua zinazohusika na Spika au maofisa wa Bunge. Ni kosa kwa mtu yeyote kutumia nembo ya Bunge kwa nyaraka binafsi," alionya.

Alisema mbunge au mtu yeyote asiyehusika, akitumia nembo hiyo kwenye nyaraka binafsi, jambo hilo litahusishwa moja kwa moja na Bunge hata kama Bunge halifahamu, kitu ambacho ni kosa la jinai.

"Sasa leo (jana) ninapiga marufuku matumizi ya nembo ya Bunge kwenye nyaraka za wabunge zinazohusu mambo yao binafsi," alisisitiza.

Ingawa Spika hakutaja jina la mbunge husika, juzi kulisambaa taarifa kwenye mitandao ya jamii ikidaiwa kutolewa na Mbunge wa Bariadi, Kundo Mathew, akitangaza nafasi za ufadhili wa masomo ngazi ya uzamili na shahada ya kwanza kwa wakazi wa Bariadi kupitia ofisi yake ya jimbo. Taarifa hiyo ilikuwa na nembo ya Bunge la Tanzania.

**UMRI WABUNGE 76**

Kuhusu taarifa za wabunge, Spika Ndugai, alisema atatoa takwimu mbalimbali kuhusu Bunge hilo, lakini hadi sasa wabunge 76 hawajawasilishwa taarifa kuhusu umri wao.

"Kwa takwimu nilizonazo, wabunge walio chini ya umri wa miaka 40, ni wachache na walio zaidi ya umri wa miaka 50 ni wachache. Sasa, wengi waliopo ni kati ya umri wa miaka 40 na 50, kwa maana hiyo Bunge hili ukiliita la vijana au wazee unakosea," alisema.

## HABARI KITAIFA

# JPM azipa siku 30 taasisi zinazodaiwa mabilioni

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

RAIS John Magufuli ametoa siku 30 kwa taasisi zinazodaiwa na Jeshi la Magereza Sh. bilioni 10 kuhakikisha zinalipa fedha hizo ndani ya muda huo.

Aidha, amesema hatasita kutoa maelekezo kwa Ofisi ya Hazina kukata moja kwa moja madeni yao na kuwasilisha fedha hizo Magereza endapo watashindwa kulipa kwa kipindi hicho.

Rais Magufuli ameonyesha kufurahishwa na utendaji wa Jeshi hilo, kwa sasa ambapo lina uwezo wa kulisha afungwa kwa asilimia 80.

Rais Magufuli alitoa kauli hiyo jana, alipokuwa akizindua Makao Makuu ya Jeshi hilo yaliyopo Msalato jijini hapa.

"Kuna madeni yanayofikia Sh. bilioni 10 ambazo mnadai kwenye taasisi mbalimbali za serikali, hili naliweza, peleka madeni yote yaliyohakikiwa kwa Waziri wa Fedha na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha kila taasisi inayodaiwa, nitawakata moja kwa moja kule Wizara ya Fedha ili fedha hizi zije," alisema.

Aliongeza "Wakati mwingine msilalamike sana vitu kidogo vifanyeni hata kwa kuwakamata na kuwaweka ndani maana fedha za posho wanalipana, za matumizi ya kawaida wanalipana, lakini madeni hawalipi," alisema.

Hata hivyo, alisema kuna viongozi wa Magereza ambao walitumia nafasi zao vibaya ikiwamo kutoa maeneo ya jeshi kinyume na taratibu.

"Kuna eneo hapa hapa kapewa mtu binafsi eneo la Magereza, lingine TANROAD, je, kulikuwa na makubaliano? Unaona harufu ya rushwa bado ipo, uwezo wa kuwaweka ndani unao, wabane watoke makamasi, mambo ya kijeshi tupeleke kijeshi ni lazima ndani ya majeshi yetu tujikosoe," alisema.

Aliongeza: "Unaenda Makao Makuu ya Jeshi unapita kwanza kwa raia na aliyefanya hivyo ni askari Magereza, hata hatua hazijachukuliwa hata jina hamjaleta nimfukuze au nimstaafishe, Kamishna una kazi ya kufanya kwenye Magereza lazima tujisahihishe, mnajichelewesha kunufaika na matunda mazuri ya kazi yetu na hawa ni wachache," alisema Rais Magufuli akionyesha kukerwa na mtu aliyepewa eneo la Magereza jirani Makao Makuu hayo.

"Yaani kila litakalofanyika yeye atakuwa anarekodi maana yake vyombo vyetu vinakosa siri kwa sababu ya tamaa ya watu wachache," alisema.

**AFURAHISHWA NA MAGEREZA**

Kuhusu utendaji wa Jeshi hilo, Rais Magufuli alisema amefurahi kwa dhati kuona Jeshi la Magereza jipya kwani linafanya kazi nzuri.

Alisema kabla ya uzinduzi huo alitembelea Gereza la Isanga na kuzindua nyumba 24 za askari Magereza ambazo kila moja inakadiriwa kugharimu Sh. milioni 25 na ni sehemu ya nyumba 213 ambazo zinajengwa maeneo mbalimbali nchini kwa takribani Sh. bilioni 7.

"Kati ya fedha hizo serikali imetoa Sh. bilioni 3.5 na kiasi kilichosalia kimetolewa na Magereza wenyewe ikiwamo nguvu kazi ya wafungwa asanteni sana magereza, huu ni mwanzo mzuri, watu walizoea ukienda nyumba za magereza ndio unakuta za ajabu ajabu, sasa mwelekeo mpya umeanza kupatikana chini ya usimamizi wako Kamishna Jenerali na hapa nazindua Makao Makuu ya Jeshi ambayo imejengwa kwa Sh. milioni 900 kwa kutumia nguvu kazi za Magereza," alisema.

Rais Magufuli alisema kutokana na kufurahishwa huko ataongeza Sh. bilioni 2.5 ili Makao Makuu ya Magereza yamalizike haraka.

"Naamini huu uwezo sasa mnao, Wizara ya Fedha kabla ya wiki ijayo haijamalizika Sh. bilioni 2.5 ziwe zimetua hapa Makao Makuu, mmenifurahisha, nina uhakika mtakubaliana na mimi nilipofanya mabadiliko na kumleta Mzee, kwa mwendo huu askari magereza hamwezi kukwama kwa sababu napenda kuona matokeo, hata sare mnazozungumza Kamshina wa Magereza aliyepita yeye ndio alikuwa msambazaji kupitia mke wake," alisema.

"Nataka niseme ukweli kwa sababu utabaki kuwa ukweli, yeye alikuwa ndio msambazaji, ukiona hatua imefikia hivyo basi jeshi halipo nikabadilisha nikaweka mwingine naye hivyo hivyo, mpoleee nikaona nimpe ubalozi akawe mpole huko."

"Ninasema ukweli kwa sababu sipendi unafiki, kwa hiyo Mzee umefanya mabadiliko kwenye jeshi, matokeo yanayoonekana yanabadilisha picha ya jeshi kila mmoja anapenda mazuri," alisema.

"Unajua ni aibu mtu amefanya kosa, halafu amefungwa na aliyefanyiwa makosa aanze tena kumlisha anapokuwa amefungwa...lakini ni ukweli kuwa wafungwa walikuwa hawatumiki vizuri, tunakuwa na wafungwa maelfu hadi leo kuna wafungwa 33,300 nimeenda Isanga pamoja na kusamehe wafungwa 265 wasinyongwe leo nimekuta wafungwa wengine 78 wanasubiri kunyongwa," alisema.

"Unaweza kujiuliza wakati mwingine uongozi ni msalaba na nimeona maeneo ya kunyongea hadi nimeogopa na inatisha."

"Nimefurahi mnajilisha asilimia 80 nataka hawa wafungwa watumike kweli kweli na katika kutumika huko wanajutia makosa yao kila dhambi ina adhabu yake, nimeambiwa tangu mwaka 2020 Machi, mmefanikiwa kuokoa Sh. bilioni 10.16, wastani wa Sh. milioni 900 kwa mwezi kwa ajili ya kuwalisha wafungwa," alisema.

Alitaka asilimia 20 iliyobaki ikamilishe vizuri kwa kufanya kazi kwa sababu wafungwa wengine wana utaalamu tofauti.

"Unaweza ukapangwa utaratibu wakalima asilimia 100 na wakazalisha ziada asilimia 20 hadi 30 mkagawana askari magereza kwa utaratibu uliowekwa maana hakuna sababu ya askari magereza mkakosa ng'ombe na maziwa, unajiuliza kwanini wachungaji wapo, wakamua maziwa wapo tena bure bila mshahara mkiwatumia vizuri hawa wafungwa na hii ndio ubunifu wa nchi zilizoendelea kuwatumia wafungwa kuzalisha mali," alisema.

Alisema ujenzi wa kiwanda hicho utalifanya Jeshi la Magereza kuwa na viwanda vikubwa vya samani vinne ambavyo vitasaidia kuokoa fedha za kigeni zinazotumika kuagiza samani nje ya nchi.

Aliagiza ofisi za serikali kuacha kuagiza samani kutoka nje ya nchi na kazi hiyo wapewe Magereza, huku akitaka waendelee kuwatumia wafungwa waliopo kwa kuwa kila mfungwa anayeingia ana ujuzi wake.



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, akikagua ajali iliyohusisha daladala na pikipiki, katika makutano ya Barabara ya Bibi Titi Mohamed na Maktaba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **CHAMPION AUCTION MART,NUTMEG AUCTIONEER&PROPERTY MANAGERS CO LTD ,DOLPHIN GENERAL BUSINESS INTERPRISES C. LTD na INDEPENDENT COURT BROKERS AND COMPANY LTD** kwa niaba ya **AccessBank Tanzania Limited** watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba,Magari na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili,Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada . Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PAMBA | CHAMPION AUCTION MART | KABADI/S,AMOS | KABADI/S,AMOS | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NO 63501 | KANGAE | 19/02/2021 |
| 2 | PAMBA | CHAMPION AUCTION MART | KALOGI/D,ROBERT | KALOGI/D,ROBERT | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | NYAMIKOMA/KABITA | 22/02/2021 |
| 3 | PAMBA | CHAMPION AUCTION MART | KANUNDO/DONARD,KAPEJI | KANUNDO/DONARD,KAPEJI | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | BUSEGA | 22/02/2021 |
| 4 | PAMBA | CHAMPION AUCTION MART | OMAR/ABDULRAHIM,ISMAIL | OMAR/ABDULRAHIM,ISMAIL | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NO 25481 | MAJENGO KAHAMA | 23/02/2021 |
| 5 | PAMBA | CHAMPION AUCTION MART | MAGERE/C,MAGWEIGA | MWITA/GIMANWA,CHACHA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NO 57057 | BUNDA MJINI | 24/02/2021 |
| 6 | PAMBA | CHAMPION AUCTION MART | KIWIA/SAMSON,EKARIST | KIWIA/SAMSON,EKARIST | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NO 57701 & 57219 | KAYENZE AND KISESA | 25/02/2021 |
| 7 | PAMBA | NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD | BUNIGINI/MASALU,EMMANUEL | BUNIGINI/MASALU,EMMANUEL | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NO 54918 | BALILI BUNDA | 19/02/2021 |
| 8 | KAHAMA | CHAMPION AUCTION MART | MABULA/M,CHARLES | MABULA/CHARLES,YOHANA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | NYAHANGA-KAHAMA | 19/02/2021 |
| 9 | KAHAMA | CHAMPION AUCTION MART | BUTAWANTEMI/M,DAUD | BUTAWANTEMI/M,DAUD | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | NYAKATO KAHAMA | 26/02/2021 |
| 10 | LUMUMBA | DOLPHINE GENERAL BUSINESS ENTERPRISES LTD | IKOHE/P,JONAS | JONAS ENTERPRISES COMPANY LIMITED | ENEO LENYE HATI LENYE EKARI TANO(5) | MLANDIZI | 19/02/2021 |
| 11 | TEMEKE | INDEPENDENT AGENCIES &COURT BROKERS LTD | WAMBURA/S,DAUDI | WAMBURA/S,DAUDI | KIWANJA CHENYE BARUA YA MAUZIANO | MKURANGA-MWANAMBAYA | 19/02/2021 |
| 12 | TEMEKE | INDEPENDENT AGENCIES &COURT BROKERS LTD | MAZENGO/CHALRES,ISAAC | MAZENGO/CHALRES,ISAAC | KIWANJA CHENYE BARUA YA MAUZIANO | ZOGOALI | 22/02/2021 |
| 13 | LUMUMBA | INDEPENDENT AGENCIES &COURT BROKER LTD | MWAKUBOMBAKI/ASONI,LEA | MWAKUBOMBAKI/ASONI, LEA | KIWANJA CHENYE BARUA YA MAUZIANO | TEGETA A | 23/02/2021 |
| 14 | LUMUMBA | INDEPENDENT AGENCIES &COURT BROKER LTD | ALLY/MAHAMOOD AHMED,FATUMA | ALLY/MAHAMOOD AHMED,FATUMA | KIWANJA CHENYE BARUA YA MAUZIANO | MBEZI MSAKUZI | 27/02/2021 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa mara usomapo tangazo hili.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya fedha taslimu papo hapo na 75% baada ya siku 14 toka siku ya mnada kufanyika na ukishindwa kulipa malipo yaliyobaki mnada utarudiwa na fedha ulizo lipa hazitarudishwa
3. Gharama za kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe, kumbuka vigezo na masharti kuzangatiwa

**MAWASILIANO**
**NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD-0754497396**
**CHAMPION AUCTION MART-0716070188**
**DOLPHIN GENERAL BUSINESS INTERPRISES C. LTD-0754448694**
**INDEPENDENT AGENCIES AND COURT BROKERS LTD-0754304547**

HABARI KITAIFA

MAHOJIANO MAALUM

# Mahakama Maalum ya Ukatili inakuja

- Ijue siri kinamama kuyumba kazini
- Dhana mpya: Kazi ni ibada na haki



Zena Ahmed Said, siku alipoapishwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, kuwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. **PICHA: MAKTABA.**

**Na Sanula Athanas,**
ZANZIBAR

SERIKALI mpya ya awamu ya nane Zanzibar Jumanne ijayo itahesabu siku ya 100 kazini. Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Zena Ahmed Said, ni sehemu ya usukani wa juu kuwezesha utendaji wa kiserikali. Je, amejipangaje?

Wanahabari chini ya kivuli cha familia ya IPP walipata fursa ya kudodosa mwelekeo wake, katika mazungumzo maalum juzi asubuhi, aliyotolea ufafanuzi kama ifuatavyo:

**SWALI: Ni takriban mwezi mmoja sasa tangu uteuliwe kushika wadhifa huu. Kipaumbele chako ni kipi hasa katika kutekeleza majukumu haya mapya?**

**JIBU:** Kipaumbele changu ni kuimarisha utendaji na nidhamu kwa watumishi wa umma. Ninaamini kwamba, tukishafaulu katika hili, mipango yetu itakwenda vizuri na itatekelezeka.

Kila mtu achukulie kwamba kazi ni ibada na kila ibada ina misingi yake ambayo inapaswa kufuatwa. Ukiifuata, utendaji wako utakuwa vizuri.

Usimwibie muda mwajiri wako. Ukiiba muda wa mwajiri ni tatizo, na hili ni tatizo kubwa kwa watumishi wengi.

Kuiba muda ni dhuluma kwa serikali kwa sababu unakuwa unapata ujira kwa kazi ambayo ulitarajiwa uifanye kwa muda uliopewa, lakini hujaifanya.

**SWALI: Wazanzibar watarajie nini kutoka kwako?**

**JIBU:** Kama nilivyotangulia kusema awali, kipaumbele chetu cha kwanza ni kuimarisha nidhamu na utendaji wa watumishi wa umma. Hii itakuwa chachu ya mengine kufanyika kwa ufanisi zaidi.

Pia nitamsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza yale yote aliyoyaahidi kwenye maeneo mbalimbali kupitia hotuba zake na mikutano mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ile hotuba yake ya kufungua Baraza la Wawakilishi.

Nitatumia uzoefu wangu kumsaidia kwenye masuala ya miundombinu na utumishi. Nimekuwa RAS na ikumbukwe kwamba ukiwa RAS, unakuwa Katibu Mkuu wa wizara zote kwenye mkoa husika. Kwa hiyo, nina uzoefu mkubwa katika hilo.

**SWALI: Umekumbana na vikwazo vipi katika kutekeleza majukumu yako haya mapya?**

**JIBU:** Kwa kweli, sijakutana na vikwazo vikubwa, mengi ya kawaida. Kote nilikopita kuna shida.

Tatizo la kwanza katika wadhifa huu, kuna watu wanakuja kwangu wanadai walitendwa vibaya, walifukuzwa kazi. Akija kiongozi mpya, wanaleta matatizo yao ofisini.

Sasa, wanaeleza matatizo yao kwa kujipendelea. Ninapofuatilia kusikiliza pande zote mbili, ninabaini alitendewa haki.

Mpaka sasa, nimepokea kesi mbili na nilipofuatilia ninaona haki ilitendeka. Ukweli ndiyo utakufanya upate haki yako na siyo vinginevyo.

**SWALI: Kwa uzoefu wako katika sekta mbalimbali ulizotumikia, ni vikwazo vipi vinawakabili wanawake kazini?**

**JIBU:** Hapa jambo la msingi ni namna wewe mwenyewe unavyojichukulia. Chukulia kwamba unaweza. Kama mtu anakuamini, kwanini wewe ujione kwamba huwezi?

Tatizo lipo katika jamii kwamba wanawake, hawawezi. Pia, kasumba iliyojengeka kwenye jamii dhidi ya kundi hilo, yaani 'wanawake hawawezi'.

Yaani kukitokea tatizo katika utendaji wa mwanamke, kinachosemwa na jamii ni 'wanawake bwana!', lakini mwanamume akikosea, linachukuliwa ni kosa lake mwenyewe na siyo wanaume wote. Tubadili mtazamo huu.

**SWALI: Lipo tatizo la ukatili wa kijinsia Zanzibar ambalo linawaathiri zaidi wanawake na watoto. Unamsaidiaje Rais kulitatua?**

**JIBU:** Nilikuwa miongoni mwa walioshiriki kikao cha Mheshimiwa Rais na wadau wa mapambano dhidi ya ukatili hapa Zanzibar. Tatizo la ukatili ni kubwa.

Moja ya mikakati tuliyoweka ni kuanzisha sehemu maalum ya kushughulikia kesi za masuala hayo ya ukatili. Mheshimiwa Rais ameshaagiza hili lifanyike, sisi ni watekelezaji wa maagizo yake.

Hili si jambo la mtu mmoja, jamii husika ihusike. Jamii isipochukua hatua dhidi ya vitendo hivyo, hatutafanikiwa.

Ushahidi katika kesi zinazohusu masuala ya ukatili umekuwa kikwazo. Jamii isikubali kupoteza ushahidi, viongozi wa dini wawe mstari wa mbele kuhubiri kupinga vitendo hivyo, ili watu watambue ukatili ni dhambi.

Hawa wanawake na watoto wakidhalilika na kuathirika kisaikolojia, tunatengeneza taifa la ajabu. Toa ushahidi hata kama mkosaji ni ndugu yako. Hata Mwenyezi Mungu amekataa ukatili na udhalilishaji.

**SWALI: Unajigawaje katika kutekeleza majukumu ya Katibu Mkuu Kiongozi na mama wa familia?**

**JIBU:** Kwa kweli wanawake tuna majukumu mengi. Kwa kulitambua hilo, mimi na mume wangu tulikaa na tukakubaliana yapi mimi nifanye na yapi yafanywe na mtu mwingine.

Kwa hiyo, tukaajiri mfanyakazi kwa ajili ya kazi ambazo mimi ni vigumu kuzifanya kwa wakati ninatekeleza majukumu ya kiserikali, lakini ninatekeleza wajibu wangu kama mama wa familia.

Kwa sasa, watoto wako shule, wako vyuoni, hivyo hakuna tatizo. Ukitumia muda vizuri, mnatengeneza familia yenye upendo.

**SWALI: Wewe ni mtu wa aina gani hasa?**

**JIBU:** ... (kicheko na tabasamu) mimi mwenyewe kwa ujumla ni mkarimu na ninamheshimu kila mtu lakini usitake nikupendelee.

Kwangu kazi ni ibada! Kuna sheria za utumishi, lazima tuzitii. Siwezi kukupendelea kwa sababu tu wewe ni ndugu yangu. Siwezi kukubali kuharibu ibada hii kwa sababu nikiharibu, ninakosa thawabu kwa Mwenyezi Mungu.

**SWALI: Ulipokeaje taarifa za uteuzi?**

**JIBU:** Kwa kweli nilipokea kwa heshima kubwa! Nafasi hii ni moja tu na watu wengi wana sifa za kupewa kazi hii, lakini Mheshimiwa Rais akaona ninafaa katika hili. Nimepokea kwa heshima kubwa!

Ninamshukuru kwa heshima kubwa. Pia, ninawashukuru wote walionilea hadi nikafika hapa. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Pombe Magufuli, nilikuwa RAS wa Tanga hadi Katibu Mkuu Wizara ya Nishati.

Nitayafanyia kazi vizuri sana haya niliyojifua huko toka mwaka 2016, nitayatumia huku. RC (Mkuu wa Mkoa) wa Tanga alinipa ushirikiano mkubwa, Mkurugenzi wa TANROADS (Wakala wa Barabara) alinipa ushirikiano mkubwa. Ninawashukuru kwa kunipa ushirikiano.

Pia mume wangu na watoto wamekuwa na mchango mkubwa kwangu.

# Wawili mbaroni utoroshaji mifugo

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

JESHI la Polisi mkoani Tanga, kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, limewakamata watuhumiwa wawili wa utoroshaji wa mifugo maeneo ya mipakani.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Blasius Chatanda, watuhumiwa hao walikamatwa kufuatia operesheni ya hivi karibuni yenye lengo la kudhibiti matukio ya wizi wa mifugo pamoja na usafirishaji wake nje ya nchi bila kufuata utaratibu.

Kamanda Chatanda alisema pamoja na kuwakamata watuhumiwa hao wawili, bado jeshi hilo linaendelea kuwatafuta wengine ambao wamekuwa wakijishughulisha na utoroshaji huo wa mifugo kinyume cha taratibu.

"Mpaka wetu wa Horohoro ni miongoni mwa mipaka inayoweza kutumika kupeleka mifugo nje ya nchi hususani nchi jirani ya Kenya na pia Bahari yetu ya Hindi nayo inaweza kutumiwa kuvusha mifugo kupeleka Tanzania Visiwani, Comoro, Ushelisheli na Madagascar," alibainisha Chatanda.

"Ndiyo maana tukaanzisha operesheni hii kabambe na katika eneo hili la Wilaya ya Mkinga kulikuwa na watuhumiwa watatu ambao walikuwa wakidaiwa kusumbua sana katika eneo hili, tumewakamata wawili ambao wameunganishwa na wengine waliokamatwa Arusha na taratibu za uchunguzi zinaendelea ili hatimaye wafikishwe mahakamani."

Alisema Mkoa wa Tanga ni kati ya mikoa yenye wafugaji wengi na kuwataka wanaojihusisha na utoroshaji wa mifugo kuacha mara moja kwa kuwa mkono wa sheria uko kazini.

"Katika mpaka wa Horohoro kwa miaka mingi mifugo ilikuwa inavushwa bila kufuata utaratibu, kwa sababu ilikuwa inapitishwa katika njia zisizo rasmi na kwenda kwenye soko la nchi jirani hali ambayo ilichangia wafugaji kuuza mifugo kwa hasara na wengine kupoteza mifugo wakati wa kuvusha kwenda huko," alisema Chatanda.

# DC aagiza watoto wa mchungaji wakamatwe, wapelekwe shuleni

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MKUU wa Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, Deodatus Kinawiro, amemwagiza Ofisa Elimu ya Msingi Manispaa ya Bukoba, kuwakamata na kuwapeleka shuleni kwa nguvu watoto watatu wa familia ya mtu anayejiita mchungaji aliyekataa kuwapeleka watoto wake shuleni, akidai kufanya hivyo ni dhambi.

Inadaiwa watoto hao ambao mkubwa wa kike mwenye umri wa miaka 13, wa pili wa kiume (9) na wa tatu wa kike (5), tangu wazaliwe, hawajawahi kupelekwa kliniki na wakiugua hawapelekwi hospitalini.

Kutokana na kuwapo kwa taarifa hizo za watoto hao kutokwenda shuleni wakizuiwa na wazazi wao wanaodai maandiko ya Mungu hayaruhusu kusoma elimu dunia, kiongozi huyo wa wilaya, akiongozana na baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, alifika katika familia hiyo kujionea hali halisi.

Licha ya kuwapa elimu kuhusu umuhimu wa watoto kwenda shuleni, wazazi waligoma kutekeleza suala hilo.

Mkuu wa Wilaya alisema baba huyo akiendelea kushirikilia msimamo wake wa kuzuia watoto kwenda shuleni, atakamatwa na kushtakiwa.

"Wanasema Biblia inasema hii shule tunayofundisha sisi ni haramu, nimesikitika, lakini nimekasirika sana, nimewaagiza wazazi na pia Ofisa Elimu Msingi wa Manispaa ya Bukoba, watake wasitake, watoto watachukuliwa waende shule, leo wakachukuliwe hata kwa kutumia polisi," aliagiza.

Baba wa watoto hao, Merchades Buberwa, aliyedai ni mchungaji wa Kanisa la Wakristo Washikao Amri za Mungu, ambalo makao yake makuu yako Mbinguni, alidai hayuko tayari kuruhusu watoto wake kutenda dhambi kwa kwenda shuleni.

"Sisi kwa mujibu wa imani yetu, Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, jinsi maandiko matakatifu yanavyosema, kwa watu wazishikao amri za Mungu, anakataza kabisa, anasema watu wamwaminio hawaruhusiwi kufundisha elimu yoyote na maandiko yapo," alisema.

Mama wa watoto hao, Agripina Maganja, alimweleza mkuu huyo wa wilaya kuwa, hata akitumia nguvu na mamlaka aliyonayo kuwapeleka watoto wao shuleni, Mungu atasimama na kuwatetea.

"Nani atawapeleka? Sisi hatuwezi kufanya hivyo na tuko tayari kwa lolote. Kama mitume walifia imani na sisi tuko tayari kumfia Mungu," alisema.

Familia ya Merchades kwa sasa ina watoto watano na wote haina mpango wa kuwapeleka shuleni.

Udadisi wa Nipashe pia ulibaini kwamba wanafamilia hao hawaruhusiwi kumiliki simu, kutazama televisheni na hawashiriki shughuli zozote za kijamii wakidai kufanya hivyo ni dhambi.



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe (wanne kulia), akipata maelezo ya mradi wa maji Jet Buza kutoka kwa Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mkoa wa kihuduma wa Temeke, Crosman Makere, baada ya kukagua mradi huo wenye thamani ya Sh. bilioni 3.7, wilayani humo juzi. Mradi huo, unalenga kuboresha huduma ya maji kwa wakazi wa maeneo ya Kiwalani, Jet, Buza na Mwanagati. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanane kortini tuhuma unyang'anyi kwa silaha

**Na Joctan Ngelly, GEITA**

WATU wanane wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita kwa kosa la unyang'anyi wa kutumia silaha kwa kuvamia kituo cha mafuta Mara, kilichoko Mtaa wa Buhalahala, Wilaya ya Geita na kuiba zaidi ya Sh. milioni 5.9.

Washtakiwa hao ni Mase Thomasi (21), Mussa Cosantine (32), Yusuph Matias (33), Peter Lucas (23), Kazimili Msuluja (32), Wilson Busalama (20), Adamu Issa (32) na Emmanuel Sospeter (22) wote ni wakazi wa Geita.

Watuhumiwa hao walifikishwa mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Sosthenes Kiiza, na walikana mashtaka hayo.

Awali, wakili wa Serikali James Pallangyo alidai hapo mahakamani humo kuwa upelelezi wa kesi hiyo yenye namba 32/2021 umekamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya usikilizwaji wa awali.

Aidha, Hakimu Kiiza alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Februari 18, mwaka huu na washtakiwa hao walipelekwa mahabusu kwa kuwa kosa lao halina dhamana.

Akisoma hati ya mashtaka mahakamani humo, Wakili wa Serikali Pallangyo, alidai kuwa Januari 29, mwaka huu, majira ya usiku katika kituo cha Mafuta Mara kilichoko eneo la Buhalahala wilayani Geita, washtakiwa wote kwa pamoja walivamia kituo hicho wakiwa na silaha mbalimbali ikiwamo mapanga, marungu na mashoka na kuiba Sh. 5,922,700.

Aidha, alisema kabla ya tukio hilo washtakiwa hao waliwafunga kamba wafanyakazi wa kituo hicho ili kufanikisha wizi huo.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Pongezi Katibu Mkuu Kiongozi kutambua kipaumbele muda

**JUZI,** Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Zena Ahmed Said, alifichua kuwapo kwa tatizo la watumishi kuiba muda wa mwajiri.

Katika mahojiano maalum na wahariri wa magazeti ya Kampuni ya The Guardian visiwani Zanzibar, Zena ambaye aligusia dosari hiyo, kwamba ni kikwazo kikuu kwa maendeleo ya nchi.

Msisitizo wake ni kuwapo mwamko mpya wenye mtazamo chanya, kwamba waajiriwa sasa waamke kwa kubeba dhana kuu mbili ambazo wakienda nazo kama jozi moja, hapana shaka maendeleo ni jambo la uhakika kwao na taifa kwa upana wake.

Katibu Mkuu Kiongozi anazitaja dhana hizo kuwa ni itikadi binafsi ya mwajiriwa kuifanya kazi iliyomwajiri kuwa sehemu ya ibada yake na wakati huo huo, kuthamini uelewa kwamba kuiba au kupotosha muda anaotarajiwa kuwajibika nao, moja kwa moja ni kuiba sehemu ya maendeleo yake.

Analifafanua hilo kwa kuitafsiri kuwa ni kanuni muhimu ya kuvuka daraja la kuelekea maendeleo, kwani dosari yoyote itakayojitokeza hadi kupoteza muda, tayari mhusika atakuwa ameshiriki moja kwa moja kukwamisha jitihada zilizoko kila upande.

Zena aliwasilisha dhana hiyo ambayo imebeba sura ya mikakati ya ofisi yake kikazi, akijivunia uzoefu wake katika utumishi wa umma kuanzia alikokuwa kwenye Wakala wa Barabara (TANROADS), Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga kisha akakwea kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati.

Kimsingi, nidhamu ya kazi kuanzia nadharia za utawala na menejimenti, inaundwa na mambo mengi mtambuka, muda na nidhamu nayo inashika nafasi muhimu kupindukia.

Itakumbukwa hata katika mfumo wa uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kwa namna ya kipekee ndani ya miaka mingi ya mikakati ya kimaendeleo, alihamasisha dhana ya 'wakati ni mali' ambayo inaangukia kwenye kile kile anachokihimiza Katibu Mkuu Kiongozi.

Vivyo hivyo, Mwalimu Nyerere alitanua wazo hilo ndani ya kuzingatia muda, kila mtu awajibikie anachopaswa kukitenda kwa wakati huo kama nukuu yake ya mwaka 1964 alipounda mpango wa kwanza wa maendeleo nchini wa mwaka mitano, akitamka 'inawezekana, timiza wajibu wako'.


Matunda ya matumizi yake yana ushuhuda mpana, ukiwamo kuundwa viwanda vingi vya uzalishaji wa ndani, mageuzi makubwa ya kilimo, elimu, sheria, fedha na hata Azimio la Arusha linaangukia katika kapu hilo.

Kwa kuanzia, Nipashe tunampongeza Zena kwa maono yake ya msingi wa awali kuivusha Zanzibar ndani ya nyenzo muhimu ya maendeleo kiuchumi, ambayo ni nguvukazi ya wananchi wake.

Tuhitimishe kwa kauli, siku zote kutambua ubia wa kazi ni uhai na wakati ni mali, ni silaha muhimu zaidi katika mkakati wa aina yoyote ile ya maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tugeuke tulikotoka kuiga uhusiano umma, serikali

Na Sabato Kasika

**NI** ngumu kukubali, lakini ndio hali halisi inayotawala. Hakuna jambo jema kama kujifunza kutoka waliofanya wengine mahali kwingineko.

Kuna wakati katika zama za uongozi wa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, alibuni mfumo mzuri sana unaohusiana na kutenda mikakati na miradi ya maendeleo kutokana na egemeo la mifumo ya kitaalamu.

Ili kujiweka sawa, uongozi wa awamu ya kwanza ya nchi ulikuwa na mfumo kila aina ya matendo uliokuwa sambamba na mwongozo wa kitaaluma kusimamia.

Na hilo limekuwa likiendeshwa kwa kina kwa namna kwamba, vinaanzishwa vyuo vipya na vilivyokuwapo viliimarishwa kwa kina, katika kujali na kusimamia mustakabali huo.

Tulishuhudia kwa mfano, vyuo vya kilimo na wataalamu wake hata ikafika uendelezaji kilimo 'neno bwana shamba' lilivyokuwa karibu sana na watu waliokuwa kila mahali na urafiki wao uliofikisha umma mbali zaidi kimaendeleo.

Mwalimu Nyerere alipokuwa mwanafunzi wao, alizuru kila mahali kutoa mafunzo ya namna mpunga unavyopadwa kwa kanuni ya umbali wa nchi moja, kutoka mbegu ilikopadwa.

Hakuna namna suala la kilimo lilivyochukua nafasi yake na kufika upeo wa juu, mazao nafaka kama mpunga, mahindi na mtama yalifika ngazi ya juu.

Vivyo hivyo, tunawakumbuka sana namna wataalamu kutoka sekta ya ustawi wa jamii walivyojipanga kuboresha mambo yao ya kijamii na mengi yakafurahiwa na jamii.

Ni aina ya uelewa ulio mtambuka kijamii, ambayo katika namna mbalimbali unahitajika katika sura pana zaidi ndani ya jamii.

Mfumo wa kitaifa, kulingana na itikadi za kasiasa, sera za kiuchumi na kimaendeleo ziliendana kwa pamoja kuibua mkakati unaowaoniua wananchi katika sura moja pana.

Kuna dhana kila zama na azma zake. Mabadiliko ya kiuongozi yamekuwa yakichukua sura katika namna inayohitaji kwenda na wakati kila kuchao maishani.

Mathalan, kadri kulivyoshuhudiwa aina hiyo ya mageuzi, aina ya mahitaji, sera, itikadi na mahitaji ya kimaisha nayo yamekuwa yakisonga zaidi katika sura mpya na inayofaa kwa wakati huo tajwa.

Ninapotamka wakati tajwa, binafsi ninafahamu jinsi kunavyoibuka jamii mpya ikihuitaji jamii ya wakati huo. Majibu ni kuwa na maendeleo yanayogusa mahitaji ya wakati kama nilivyotamka awali.

Zamani upande wa pili kwa maana ya jamii, nao ina wajibu wa kuwa na mwamko mkubwa katika juhudi za kuendana na mahitaji tajwa, vivyo hivyo wataalamu kuwa karibu.

Kuna baadhi ya maeneo huwa nabaki katika masikitiko makubwa, pale ninapoona mathalan kuna mbawana shamba wanaobaki kuwa maofisa wa ofisini, huku wakazi wao nao hawajui mabwana shamba walivyo. Jambo la kusikitisha sana.

Ndio simulizi inayoenda mbali, watu hao wawe maofisa kilimo na waliopo katika ustawi jamii, umaarufu na uelewa wao unabaki katika ngazi ya pale inapoibuka shida kama ukame dhidi ya kilimo, au mimba za mabinti mtaani.

Wataalamu kama walimu na madaktari, ndio wanaobaki kuwa wasifu mkubwa na hata wakajulikana kupitiliza, maana wameshikilia aina mbalimbali za shida kuu za kijamii.

Msingi unaopaswa kufanyiwa kazi na kuzingatiwa ni jamii kugeuza visogo na kutathmni walikotoka zama hizo za miaka ya 1970 na kabla, hadi ukomo wa mwaka 1985, mbinu ya uwiano wa pamoja pande zote unaumuhimu kupindukia.

# Kanisa lasisitiza hadhari magonjwa ya mlipuko

**Na Said Hamdani, LINDI**

KANISA la Anglikana Mkoa wa Lindi, limewashauri waumani wake kuchukua tahadhari kwa kunawa mikono kwa maji tiririka, kabla na baada ya kuingia ndani ya kanisa na kukaa kwa nafasi.

Tahadhari hiyo imetolewa na mchungaji wa Jimbo hilo la Lindi, Yusuphu Falotino, wakati akizungumza na waumini wa kanisa hilo katika kikao maalum cha kupanga mikakati ya kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona mjini humo.

Alisema ni muhimu waumini hao wakafuata taratibu za kujikinga ikiwamo kuepuka safari zisizo za lazima, kuepuka misongamano na kuvaa barakoa, kwa kuwa ugonjwa wa corona unaisumbua dunia.

Kiongozi huyo wa Kanisa la Angalikana Jimbo la Lindi, aliwasisitiza waumini kuzingatia vyema maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya jinsi ya kujikinga na ugonjwa huo hatari hapa duniani.

Alisema tayari uongozi wa kanisa umeshachukua tahadhari kwa vitendo, ikiwa ni pamoja na kuandaa vifaa muhimu vinavyohitajika kutumiwa na waumini wao kama inavyosisitizwa na wataalamu wa afya.

"Ninachowashauri waumini wote kuanza kuchukua tahadhari ikiwamo kuvaa barakoa na kufuata kanuni za kukaa kwa kupeana nafasi," alisema Mchungaji Falotino.

Prisca Yohana Unga na Richard Shabani ni waumini wa kanisa hilo la Anglikana Jimbo la Lindi, walisema wameupokea ushauri wa kiongozi huyo na kwamba watachukua tahadhari.

Naye Mkandarasi Selemani Kinjikitile, alisema ni vizuri jamii ikachukuwa tahadhali, kama kanuni za afya na maelekezo yanayotolewa na viongozi wa dini wanavyotahadharisha kwenye nyumba za ibada.

# Huduma 'Daktari Nyumbani' yazinduliwa

**Na Frank Monyo**

HOSPITALI ya Aga Khan nchini, imezindua huduma ya kwanza ya kuwasiliana na daktari ukiwa nyumbani kwa kutumia simu ya mkononi "Pigia Daktari App" ili kupunguza muda wa kupata huduma kwa mgonjwa pamoja na kuonana na daktari kwa haraka.

Akizungumza katika uzinduzi wa huduma hiyo uliofanyika jana, jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Huduma za Afya Aga Khan, Sisawo Konteh, alisema huduma hiyo itamwezesha mgonjwa kupata huduma bora za afya kutoka kwa madaktari bingwa bila kufika hospitali pia na kupunguza muda wa kupata huduma.

Alisema "Pigia Daktari App" pia itamwezesha mgonjwa kuweka ahadi ya kuonana na daktari bingwa au kupata huduma hasa kipindi hiki cha maambukizi ya ugonjwa hatari wa homa ya mapafu wa COVID-19.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa huduma hiyo ni ya kwanza nchini na itasaidia kurahisisha upatikanaji wa huduma za matibabu kutoka kwa madaktari bingwa kutoka katika hospitali zote za Aga Khan kwa urahisi.

"Tuna upungufu wa madaktari bingwa hivyo kupitia huduma hii itawezesha wagonjwa kuwasiliana na wataalamu wetu mahali popote walipo bila ya wao kuja kupanga foleni kuonana na daktari bingwa," alisema Konteh na kuongeza:

"Huduma hii ya kuwasiliana na daktari kiganjani mwako ni ya kwanza kwa hapa Tanzania, na huduma hii itaweza kutumika na mtu yeyote popote alipo kwenye hospitali zetu za Aga Khan na mgonjwa akapata huduma akiwa nyumbani na kupunguza muda wa kupata matibabu."

Aliongeza kuwa "Pigia Daktari App", itasaidia wagonjwa ambao wanashindwa kufika hospitali ama kwa kukosa nguvu au kuzidiwa. Pia akashauri kuwa kwa wale wenye magonjwa makubwa yanayohitaji huduma ya haraka wanatakiwa kufika hospitali na sio kutumia huduma hiyo.

"Yapo magonjwa yanayohitaji huduma za matibabu za haraka, hawa wafike hospitali na sio kutumia "Pigia Daktari App" kwa mfano mtu akipata ajali huyu anatakiwa kufika hospitali mapema kupatiwa huduma."

Akizungumza kwa niaba ya serikali, Mkuu wa Chuo cha Afya cha Afrika Mashariki kinachomilikiwa na Aga Khan, Profesa Hussein Kidanto, alisema kuwa huduma hiyo inatoa nafasi ya kupunguza mzigo kwa watoa huduma ya afya.

"Pigia Daktari App" itasaidia kupunguza muda wa kusafiri kufika katika hospitali, pamoja na kuhifadhi siri za mgonjwa na daktari wake na kukupa muda wa kuchagua daktari bingwa kulingana na matibabu," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Huduma za Afya Hospitali ya Aga Khan, Sisawo Konteh (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa huduma ya kwanza kwa njia ya mtandao ya "pigia daktari App". Kushoto ni Mkuu wa Maendeleo ya Biashara wa hospitali hiyo, Mili Rughani na Meneja Mwandamizi, Masoko na Mawasiliano, Olayce Lotha. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanawake wakwaa nafasi za uongozi

**Na Romana Mallya**

WANAWAKE 150 walionufaika na mafunzo ya Mwanamke Kiongozi (Female Future) yaliyozinduliwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, yamewawezesha baadhi yao kupanda vyeo kwenye taasisi zao wanazozifanyia kazi.

Mafunzo hayo ambayo yalizinduliwa miaka mitano iliyopita lengo lake lilikuwa ni kuwandaa kufikia nafasi za juu za uongozi na kupata fursa ya kuingia kwenye bodi na kushiriki katika kutoaji uamuzi.

Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Dk. Aggrey Mlimuka, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano mkuu wa tatu wa wanawake katika uongozi unaotarajia kufanyika mwezi ujao.

Alisema mkutano huo utafanyika sambamba na mahafali ya 4, 5, na 6 ya programu hiyo ya Mwanamke Kiongozi.

Dk. Mlimuka alisema wanawake kadhaa waliohitimu mafunzo hayo ambayo hutolewa kwa miezi tisa, wamenufaika kwa kupata nafasi za juu za uongozi na kuwa wawakilishi kwenye bodi na mchango wao ukionekana dhahiri.

Kuhusu mkutano huo wa mwaka wa tatu alisema utabebwa na kauli mbiu isemayo, "Ukuzaji wa vipawa vya wanawake walio katika uongozi ili kuwa na mashirika endelevu."

"Lengo lake ni kuwaleta pamoja viongozi wa kampuni, mashirika binafsi na ya umma, mashirika ya kimataifa na kitaifa, taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa na mabalozi wanaowakilisha nchi zao hapa Tanzania ili kujadili namna nzuri ya ujumuishwaji wanawake katika nafasi za juu za uongozi," alisema.

Alitaja malengo makuu ya mkutano huo wa pili wa wanawake na uongozi kuwa ni kuongeza ufahamu kuhusiana na faida za kuwa na usawa wa jinsia katika eneo la kazi.

"Kubadilishana ujuzi na uzoefu, kushuhudia na kusherehekea mafanikio yaliyotokana na programu ya wanawake kiongozi tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016 na kujadili changamoto zao," alisema.

Pia alisema siku hiyo wadau watapata nafasi ya kusisitiza umuhimu wa ushirikishwaji wa wanaume katika maeneo ya kazi ili kuongeza uwezeshwaji wa wanawake kiuchumi.

# Mimba za utotoni, wapenzi wengi chanzo cha saratani

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

DAKTARI wa Idara Magonjwa ya kinamama katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, Dotto Dede, amebainisha chanzo cha saratani ya mlango wa shingo ya kizazi kwa wanawake mkoani Shinyanga, kuwa mimba za utotoni, kuwa na wapenzi wengi na kuzaa mfululizo bila ya kuacha nafasi.

Dede alibainisha hayo jana, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Saratani Duniani, kuwa katika Mkoa wa Shinyanga saratani ya mlango wa shingo ya kizazi, ni tatizo kutokana na uelewa mdogo wa wanawake kuepukana na maradhi hayo.

Alisema katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Shinyanga, kila wiki wanapokea wanawake wawili ambao wanatatizo la saratani ya mlango wa shingo ya kizazi, na wale ambao wanakutwa wakiwa katika hatua mbaya huwapa rufani ya kwenda kutibiwa Hospitali ya Bugando jijini Mwanza.

"Saratani ambayo ni tatizo kwa wanawake mkoani Shinyanga ni shingo ya mlango wa kizazi, na hii inatokana na sababu ya kukithiri kwa mimba za utotoni, ambapo via vya uzazi vinakuwa bado havijakomaa, kuwa na wapenzi wengi, pamoja na kuzaa watoto mfululizo bila ya kuacha nafasi," alisema Dede.

"Mwanamke unapokuwa na wapenzi wengi ni virahisi sana kuambukizwa virusi vya (HPV), ambavyo husababisha kupata saratani ya mlango wa shingo ya kizazi, pia uzazi wa mfululizo watoto husababisha kizazi kulegea na rahisi kupata matatizo hayo ya saratani," aliongeza.

Pia alitaja baadhi ya dalili za saratani ya shingo ya kizazi, kuwa ni kutokwa damu na uchafu sehemu za siri baada ya kumaliza kufanya tendo la ndoa, pamoja na kukojoa damu, huku akiwataka wanawake kujenga tabia ya kupima afya zao, ili wawahi huduma ya matibabu, na siyo kwenda kutibiwa wakiwa katika hatua mbaya.

Mmoja wa wanawake ambaye alikwenda kupima saratani ya shingo ya kizazi, Mary Kalinyi, alisema baada ya kusikia kuna huduma ya upimaji aliamua kupima ili kujua afya yake.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu utendaji wa benki hiyo, katika kipindi cha mwaka 2020. Kushoto ni Mkuu wa Idara ya Mikopo wa benki hiyo, Zainab Nungu na Ofisa Mkuu Idara ya Fedha, Shani Kinswaga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# CCM yajitosa ujenzi madarasa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Shinyanga, kimechangia mifuko 10 ya saruji kwa ajili ya kusaidia kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa, katika Shule ya Sekondari Ngokolo iliyopo Manispaa ya Shinyanga.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, alikabidhi mifuko hiyo juzi kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Ngokolo, Malale Sawaka, huku akiahidi mifuko 10 ya saruji na kufanya jumla yake 20.

Alisema katika ziara hiyo ya Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Shinyanga, waliridhishwa na ujenzi wa vyumba vya madarasa katika baadhi ya shule mjini humo.

"Katika ziara hii tumeridhishwa na kasi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, ila nitoe rai kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, kujipanga kutatua changamoto ya upungufu wa viti, meza na madawati, ili wanafunzi wasikae chini," alisema Mlolwa.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, aliwataka wananchi kuendelea kujitoa kuchangia shughuli za maendeleo, hasa ujenzi wa vyumba vya madarasa ili serikali imalizie majengo hayo.

Kwa upande wa Mkuu wa Shule ya Sekondari Ngokolo, Malale Sawaka, alisema katika shule hiyo wana jenga vyumba vinne vya madarasa, na vipo katika hatua ya ukamilishaji, ili ifikapo mwishoni mwa mwezi huu, wanafunzi ambao walikosa nafasi kujiunga na kidato cha kwanza waanze kusoma.

Aidha, katika taarifa ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Geoffrey Mwangulumbi, alisema shule za msingi zinakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 64, sekondari 34.

Awali katika taarifa yake, Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, Mohamed Kahundi, alisema kuna upungufu wa vyumba vya madarasa 5,881, madawati 16,672, huku wanafunzi 234 wakikosa nafasi za kujiunga kidato cha kwanza.

# Wanufaika TASAF waishukuru serikali

**Na Richard Makore,** MAGU

ZAIDI ya wanufaika 5,000 wa ruzuku inayotolewa na serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Nchini (TASAF), wilayani Magu mkoani Mwanza wameipongeza serikali kwa namna inavyowajali na kusaidia kuwakomboa kutoka kwenye umaskini.

Akizungumza juzi katika ziara ya kuwatembelea wanufaika hao ambazo ni kaya maskini, Ofisa Ufuatiliaji wa TASAF wilayani Magu, Linna Marealle, alisema ruzuku hiyo imezisaidia kaya maskini kujikwamua kiuchumi.

Alisema kabla ya kaya hizo kuanza kupatiwa ruzuku na TASAF zilikuwa zikiishi maisha magumu na kwamba hivi sasa zinaishi maisha kama ya watu wengine ikiwamo kumudu kupata chakula, kugharamia huduma za afya pamoja na kusomesha watoto wao.

Aliongeza kuwa mpaka sasa wanufaika hao zaidi ya 5,000 wanatoka vijiji 62 kwa wilaya nzima ya Magu na kwamba kila baada ya muda wanawatembelea ili kuona maisha wanayoishi.

Kwa upande wake, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Ndagula, wilayani Magu, Stella Joseph, alisema baada ya wanufaika kupata ruzuku wanawatembelea na kuwashauri waunde vikundi ili kuanzisha shughuli za uzalishaji mali.

Aliongeza kuwa wao kama wataalamu pamoja na maofisa ugani wanawatembelea wanufaika hao ili kuhakikisha ruzuku wanayopewa inawasaidia kujikwamua kiuchumi.

Mmoja wa wanufaaika wa fedha hizo za TASAF, Veronica Rashid, alisema alianza kupewa Sh. 44,000 mwaka 2015 na kwamba kiasi hicho cha fedha kimeweza kumsaidia kujenga nyumba ya bati.

Aidha, aliyataja manufaa mengine aliyoyapata kuwa ni pamoja na kusomesha wajukuu zake kwa ngazi ya shule ya msingi na sekondari.

# Mamia wapimwa macho, sukari, 'presha,' saratani

**Na Joseph Mwendapole**

WANANCHI wengi wamejitokeza kupimwa macho, sukari na shinikizo la damu kwenye kambi maalum inayoendeshwa na Hospitali ya Kairuki Mikocheni na Manispaa ya Ubungo jijini Dar es Salaam.

Kambi hiyo iliyoanza Jumatano wiki hii katika kituo cha mabasi cha Mbezi Luis inatarajiwa kufungwa leo na Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisare Makori.

Baadhi ya huduma zinazotolewa kwenye kambi hiyo ya siku nne ni upimaji wa macho, sukari, shinikizo la damu, elimu ya lishe bora, dalili za awali za saratani ya matiti, kuchangia damu na elimu ya umuhimu wa bima ya afya.

Mwanabinti Hamis ambaye ni mmoja wa waliopata huduma ya upimaji wa sukari na shinikizo la damu, aliishukuru Hospitali ya Kairuki na Manispaa ya Ubungo kwa kutoa huduma hiyo bure na kushauri utaratibu huo uwe endelevu.

Alisema wananchi wengi wanashindwa kwenda kupima afya zao na kupata elimu kuhusu namna ya kujikinga na maradhi ya kuambukiza kwa kuwa wengi wao hawana uwezo wa kugharamia vipimo kwenye hospitali.

"Nimepima sukari iko juu na kabla ya hapa sikuwa najua kwasababu sikuwahi kupima ila niliposikia Kairuki wanapima bure ndipo nikawahi mapema na kweli nimehudumiwa pamoja na vipimo vya presha ambayo wamesema iko kawaida," alisema.

Mkazi wa Kimara, Mohamed Issa aliyepimwa saratani ya matiti aliwataka wanaume wajitokeze kwa wingi kupima ugonjwa huo na kuachana na dhana iliyojengeka miongoni mwao kuwa ugonjwa huo huwapata wanawake pekee.

"Nimepima nimeambiwa niko vizuri hivyo ni vyema ukapima afya yako kujua kama uko salama, ukipima na ikagundulika kwamba uko salama haikugharimu kitu kuliko ukadhani uko salama kumbe saratani ya matiti inakutafuna kidogo kidogo na huduma yenyewe hapa ni bure," alisema.

Kaimu Meneja Uhusiano na Masoko wa hospitali hiyo, Arafa Juba, alisema kambi hiyo hufanyika kila mwaka kwa ajili ya kumuenzi mwanzilishi wa hospitali hiyo, hayati Prof. Hubert Kairuki.

# Mbunge ataka uchunguzi zahanati

**Na Yasmine Protace,** KIBAHA

MBUNGE wa Jimbo la Kibaha Vijijini (CCM), Michael Mwakemo, ameeleza kutoridhishwa na taarifa za ujenzi wa zahanati ya Ruvu Stesheni na kutaka hatua zichukuliwe kuwabaini waliouhujumu.

Mwakemo aliyasema hayo, mara baada ya kutembelea mradi wa ujenzi wa zahanati ya Kijiji cha Ruvu Stesheni na kukutana na harufu ya udanganyifu ikiwamo ujenzi uliogharimu Sh. milioni 167.6 zilizolipwa fidia na Shirika la Reli, baada ya kubomoa zahanati hiyo.

Akizungumza na wanakijiji, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Martine Ntemo na madiwani wa viti maalumu, alimtaka Ntemo kuitumia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ili kubaini madudu ambayo yameleta sintofahamu kwake na kwa wananchi kuhusu zahanati hiyo. "TAKUKURU waje wafuatilie huu mradi ambao umeleta sintofahamu kwa wananchi na kwangu, baada ya kigugumizi kwenye ujenzi uliogharimu Sh. milioni 167.6 zilizolipwa fidia na Shirika la Reli (TRC), baada ya kubomolewa zahanati ili kupisha umeme mkubwa wa treni ya mwendokasi," alisema.

Aliongeza kuwa katika mradi huo, ameshangaa kusikia kuwa lori la mchanga limenunuliwa kwa Sh. 95,000, wakati mchanga huo kijijini hapo unauzwa Sh. 65,000.

Aliongeza kuwa changamoto nyingine ambayo imejitokeza katika mradi huo ni nondo zilizonunuliwa maeneo ya mbali, wakati maeneo hayo yana kiwanda kikubwa kinachozalisha nondo.

Alitaja ununuzi wa mawe, wakati yamezagaa na walitakiwa kuyaokota kuliko kwenda kununua mapya na kuongeza kuwa mradi huo fundi anakuja na vibarua wake, wakati kijijini hapo walikuwapo.

"Serikali ina sheria zake, miradi inayoanzishwa mafundi wanatakiwa kuwa wa hapo katika eneo la mradi na si kuwachukua maeneo mengine," alisema.

Mbunge huyo alitembelea mradi wa kujenga tangi la maji Kijiji cha Ruvu ambao unatekelezwa na RUWASA Kibaha na kuridhishwa na mradi huo.

Alimtaka mkandarasi aongeze kasi ya ujenzi ili adhima ya serikali ya kumtua ndoo mwanamke izae matunda.

Katika kikao alichofanya na wananchi walimwomba mbunge huyo, kufikisha kilio chao bungeni ili serikali itatue kero sugu ya wafugaji, kutokana na mifugo kuingia katika mashamba yao na kuharibu mazao yao ya chakula na biashara.



Meneja wa Taasisi ya Utafiti wa zao la kahawa (TaCRI) Kanda ya Ziwa katika mji wa Sirari, Almas Ahmad, akitoa maelezo kwa wakuu wa wilaya za mkoa wa Mara waliotembelea mashamba ya zao hilo, wilayani Tarime, jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# 'Stendi ya Kibaha ifanye kazi saa 24'

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MADIWANI wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha wameomba kufanyika maboresho katika stendi ya mabasi ya Kibaha kwa kuiongezea taa pamoja na kuwekwa huduma za kifedha na kuiwezesha kufanya kazi saa 24 badala ya ilivyo sasa ambapo ikifika saa 2:00 usiku hakuna magari yanayoingia na imefungwa.

Diwani wa Picha ya Ndege, Karimu Mtambo, alitoa ushauri huo kwenye kikao cha baraza la madiwani kilichofanyika wiki hii kujadili na kupitisha mapendekezo ya bajeti katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Mtambo alisema kwasasa mabasi makubwa yanayopita kuanzia saa 4:00 hayaingii katika stendi hiyo ambayo tayari imefungwa hivyo halmashauri kukosa mapato yanayotokana na ushuru.

Alisema endapo maboresho yatafanyika kuanzia kwenye taa ndani ya stendi hiyo pamoja na kuweka huduma mbalimbali yataifanya kufanya kazi muda wote mbali ya ajira kwa vijana wanaofanya biashara, lakini mapato ya ushuru yataendelea kukusanywa.

Akizungumzia upande wa soko la kisasa linalojengwa karibu na stendi hiyo, diwani huyo alisema utaratibu unatakiwa kuandaliwa mapema soko hilo litakapokamilika na kuanza kufanya kazi lisifungwe ili kuwezesha wasafiri na watu wengine kuingia muda wote kupata huduma.

Naye Diwani wa Mailimoja Ramadhani Lutambi, amemtaka Mkurugenzi wa Halmashauri kufanyia kazi suala la mashamba pori ambalo linachangia uwepo wa kesi za uvamizi.

Lutambi alisema baadhi ya wamiliki wa mashamba hawayaendelezi kwa muda mrefu na hivyo kuwafanya wananchi kuvamia na kugawiana pasipo kufuata utaratibu ili kupunguza vitendo vya uhalifu ambapo watuhumiwa hutumia mapori kujificha.

Halmashauri hiyo kwa mwaka 2021/2022 inakadiria kukusanya Sh. bilioni 36 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato.

Akisoma hotuba ya mapendekezo ya makadirio ya mapato ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo ya halmashauri hiyo, Makamu Mwenyekiti, Selina Wilson alisema kutoka katika mapato ya ndani wanategemea kukusanya shilingi bilioni 3.9 na ruzuku kutoka serikali kuu wanategemea kupokea shilingi bilioni 31.7.

Selina alisema kati ya fedha hizo mishahara ni Sh. bilioni 22.2, miradi ya maendeleo ni Sh. bilioni 8.1 na matumizi mengine Sh. bilioni 1.2.

HABARI BUNGENI

# TAMISEMI yataka ajira zinazozingatia kijinsia

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeziagiza halmashauri zote nchini kufanya usawa kwa walimu wa shule za msingi na sekondari kwa kuzingatia jinsia.

Aidha, serikali imesema ipo kwenye mpango wa mwisho wa kutoa ajira mpya kwa walimu. Hayo yalisemwa jana bungeni, wakati wa kujibu swali la Mbunge wa Viti Maalum(CHADEMA), Kunti Majala, aliyetaka kujua serikali itapeleka lini walimu wa kike katika shule za msingi Birise na Donsee ambazo hazina walimu wanawake.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, David Silinde, alisema na kuongeza kuwa utaratibu wa kuajiri walimu mara kwa mara unaendelea.

Alisema kwa sasa serikali ipo kwenye mpango wa mwisho wa kutoa ajira mpya kwa walimu na suala hilo litazingatia jinsia ili kuwasaidia watoto wa kike wanaohitaji walimu wanawake.

Alisema serikali inatambua tatizo la ukosefu wa walimu wa kike katika shule za msingi Birise na Donsee zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, Mkoa wa Dodoma.

Aliongeza kuwa katika kukabiliana na tatizo hilo Halmashauri ya Wilaya ya Chemba imempeleka mwalimu wa kike katika Shule ya Msingi Donsee wakati ikiendelea kukamilisha taratibu za kumpeleka mwingine Shule ya Msingi Birise.




Habari na Augusta Njoji



Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa akichangia hotuba ya Rais bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kyela sasa kunywa maji ya Ziwa Nyasa

WAKAZI wa Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya watapata maji kutoka Ziwa Nyasa, ambacho ni chanzo cha kudumu cha kusambaza maji kwa wananchi waliopo eneo hilo na mikoa jirani.

Bunge limeambiwa kuwa ili kufikia hatima hiyo, timu ya kitaifa ya wataalamu imefanya upembuzi wa awali kwa kufika Kyela na kubaini eneo la kijiji cha Ikombe kilichoko katika mwambao wa Ziwa Nyasa kuwa linafaa kujengwa chanzo cha maji.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kyela (CCM), Ally Mlaghila.

Katika swali lake, alisema suluhisho la tatizo la maji katika Wilaya ya Kyela ni kutumia chanzo cha Ziwa Nyasa kama ilivyoelezwa kwenye ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020.

"Je, ni lini sasa mradi huo utaanza kutekelezwa?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri alisema mradi huo unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2021/22, alikiri kuwa serikali inatambua tatizo la huduma ya maji linaloikabili Wilaya ya Kyela katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi, salama na ya kutosha.

"Serikali ina mpango wa muda mfupi na mrefu ikiwamo kutekeleza mpango wa muda mfupi imeendelea na ukarabati wa miradi ambayo baadhi ya miradi iliyokarabatiwa tayari inatoa huduma hiyo," alisema.

Pia alisema mradi wa maji wa kikundi cha Makwale ambao unahudumia vijiji vya Ibale na Makwale, mradi wa maji wa Matema unaohudumia kijiji cha Matema (kitongoji cha Ibungu) na Kijiji cha Ikombe (Kitongoji cha Lyulilo) na mradi wa maji wa Lubaga ulioharibika muda mrefu umekarabatiwa na wananchi wanapata maji kwenye vituo 15 vya kuchotea maji.

Aidha, alisema bajeti ya 2020/21 serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji wa Mababu, Kisyosyo, Katumbasongwe, mradi wa Kapapa kwenda kijiji cha Mwaigoga na Sinyanga.

# Bandari ya uvuvi kunufaisha 30,000

WAZANZIBARI takribani 30,000 wanatarajiwa kupata ajira baada ya kukamilika ujenzi wa bandari ya uvuvi visiwani humo.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, aliliambia bunge jana alipokuwa akijibu swali la mbunge wa viti maalum(CCM), Angelina Adam Malembeka.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema kuna mpango wa kujenga bandari kubwa ya uvuvi inayoelezwa kuwa itatoa ajira 30,000. Je, ajira kwa upande wa Zanzibar zitakuwa ngapi? Alihoji.

Gekul akijibu swali hilo, alisema uamuzi wa kujenga bandari ya uvuvi ni miongoni mwa vipaumbele vya kitaifa kama ilivyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu 2020/21 hadi 2025/26, na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, ambazo kwa pamoja zinaielekeza serikali kujenga bandari ya uvuvi.

"Kuwapo kwa bandari ya uvuvi kutawezesha meli zinazovua bahari kuu kutia nanga kushusha samaki na mazao ya uvuvi, kuuza samaki, kutoa takwimu sahihi na kupata huduma za kujaza mafuta, maji, vyakula na matengenezo ya zana za uvuvi," alisema.

Alibainisha kuwa kukamilika kwa ujenzi wa bandari ya uvuvi kunakadiriwa kutoa ajira zaidi ya 30,000 kwa Wazanzibari. "Serikali itahakikisha kuwa Watanzania kutoka pande zote nchini wanaendelea kunufaika na fursa za ajira, biashara ya mazao ya uvuvi na uwekezaji katika viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi," alisema.


Aliliambia bunge kuwa uwekezaji huo utachangia, kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya uvuvi hususan kutoka ukanda wa bahari, fedha za kigeni, mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la taifa, la mtu mmoja na mmoja na lishe.

"Katika kutekeleza mpango huo, serikali inaendelea kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari hiyo ambapo uchambuzi wa awali umetoa mapendekezo ya kujengwa kwa bandari hiyo katika eneo la Mbegani, Bagamoyo lililopo katika mwambao wa Bahari ya Hindi," alisema.



Ukurasa 14

Mhariri Mkuu: COVID-19 iliniingiza darasani kujua nguvu ya teknolojia




Ukurasa 13

Watanzania Uviko hakuna, je, mengine?



Ukurasa 12

WAZIRI MKUU MAJALIWA:

**Tunaingia miguu miwili kwenyemkonge, walimaji wadogo ni uhakika njia nyeupe**


# BUFE

IJUMAA FEBRUARI 5, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


BIASHARA

# Mtandao aina yake unaoajiri na kufanya biashara, hawaonani

• Watumiaji intaneti wako nusu ya simu

**Na Anaeli Mbise**

WAKATI idadi ya wanaotumia intaneti ikiongezeka duniani, watu walio na ujuzi wa Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nao wanahitajika kuwezesha kuunganisha watu kila waliko, kwa mujibu wa Ripoti ya Muungano wa Kimataifa wa Mawasiliano (ITU).

Ripoti hiyo inyoitwa "Kupima Mawasiliano Katika Jamii 2018" inaonyesha gharama ya TEHAMA imepungua kimataifa katika kipindi cha mwongo mmoja.

Sera ya usimamizi wa TEHAMA zinatajwa kuwa kichocheo cha kutengeneza mazingira ya kupunguza bei na kuhakikisha faida zinawafikia wahudumiaji na wateja.

"Mwaka huu ripoti inaonyesha jinsi ya kuwekeza katika teknolojia ya 'Broadband' kunaleta mabadiliko ya kidigitali kimataifa na kuwezesha watu kufikia huduma mbalimbali kwa njia rahisi," anasema Mkurugenzi Mkuu wa ITU, Houlin Zhao, alipofunga kongamano la Muungano wa Kimataifa wa Mawasiliano, jijini Dubai.

Kunatajwa faida na hasara ya TEHAMA ndani ya jamii, ingawa wataalamu wa upande wa pili wanaelezea vikwanzo vyake. Dk. Faustine Ndugulile, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, anasema kuna mambo yanayofanyika kurahisisha utoaji huduma za TEHAMA kwa wananchi, wakiwamo wafanyabiashara ambao ndiyo walipa kodi wakuu.



Ofisa Mtendaji Mkuu na Mbunifu wa Jukwaa la Mtandaoni la Gigspace, Ashura Babi, akihojiwa na mwandishi wa makala hii (hayupo pichani ). **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

Sehemu ya malalamiko yanayotolewa na wateja dhidi ya kampuni za simu juu ya vifurushi vya intaneti, vinavyotolewa haviendani na ubora wa huduma hiyo. Ni hali inayomfanya Waziri Dk. Ndugulile, kutoa agizo kwa marekebisho, alipofika katika ofisi za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kulimaliza tatizo hilo.

Takwimu za TCRA zinaonyesha kuwapo zaidi ya Watanzania milioni 51.29 wanaotumia simu, lakini ni wastani wa milioni 28 tu ndiyo wanaotumia intanenti.

Pamoja na upungufu katika idadi ya watumiaji intaneti, lakini kwenye ukweli wake, ndiko panakopatikana fursa kamili.

**WABUNIFU MRADI**

Ofisa mtendaji mkuu na mbunifu wa jukwaa la Gigspace, Ashura Babi, kwa kushirikiana na mwanzilishi mwenza wa jukwaa hilo, Steve Mawalla, wameamua kubuni wazo la kimtandao, mahususi kwa ajili ya fursa zitokanazo na jukwaa hilo.

"Lengo kuu la jukwaa ni kuunganisha mfanyakazi ambaye ana kazi, ila anakuwa anafanya kazi akiwa huru mtandaoni, pamoja na ambao hawana ajira wanajisajili kwa fani zao na tunawaunganisha na kampuni za kibiashara na wanatimiza malengo ya maisha yao," anasema Ashura.

Anaendelea: "Hii ni fursa ya watu ambao wanafanyakazi kujiongezea kipato cha ziada na wale ambao hawana ajira kupato kipato pia. Kazi zinakuwa huru ndani ya jukwaa letu ni muda mfanyakazi tu kutenga vizuri, ili atimize kazi zinazokuwa zimepatikana kupitia jukwaa la Gigspace,".

"Hii ni njia inayompa mtu nafasi ya kuendeleza ujuzi zaidi katika taaluma yake kupitia njia ya kisasa ya kidigitali, ambayo mteja anajisajili kupitia tovuti yetu ya jukwaa la Gigspace," anasema Mawalla. Hadi sasa anasema kuna jumla ya watumiaji 400 wa mtandao wa jukwaa hilo ambalo liko katika hatua za ukuaji.

Baadhi ya kada za taaluma ambazo zimesajiliwa na jukwaa hilo, zinatajwa kuwa ni pamoja na wahandisi, wahasibu, wasanifu na wabunifu wa majengo, wanahabari pamoja na watunga sera za biashara.

"Nishauri vijana wenzangu tusiridhike na kile kidogo tunachopata kupitia kazi zetu za ofisini kwa maana kutafuta kipato nje ya ofisi, inasaidia kukuza uchumi wetu. "Lakini nitoe wito kwa watu kuacha uvivu na kujiingiza katika biashara za mtandaoni maana inalipa," anasema Ashura, akiorodhesha faida na hasara zake.

**FAIDA ZA JUKWAA**

* Kupunguza changamoto ya kazi.
* Kubana matumizi ya ofisini.
* Nafasi ya wafanyakazi kuwajibika waliko.
* Kuepuka ukatili wa kingono kazini.
* Wenye mahitaji maalum kama walemavu, wana msaada.
* Inasaidia wajasiriamali wadogo kukuza biashara zao.

**HITILAFU ZA JUKWAA**

* Utayari wa watu kujiunga na jukwaa hilo la Gigspace.
* Uelewa wa watu wa namna ya kufanya biashara kimtandao.
* Matumizi mabaya ya mtandao kwa baadhi ya vijana.
* Suala la mpangilio wa muda kwa baadhi ya wafanyakazi.

BIASHARA

WAZIRI MKUU MAJALIWA:

# Tunaingia miguu miwili kwenye mkonge, walimaji wadogo ni uhakika njia nyeupe

## • Enzi za umaarufu mkonge kurejeshwa • RC Malima aweka rasmi Mara imo • Tanga kinara wa wadau mikoa mitano

**Na Mashaka Mgeta,** TANGA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wa pili kulia), akipokea maelezo ya Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo (TARI) cha Mlingano kilichopo Muheza, mkoa wa Tanga, Dk. Catherine Senkoro (wa tatu kulia). Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigella (kulia) na kwanza kushoto ni Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe. **PICHA ZOTE: MPIGA PICHA WETU**

BABA wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, katika aliyoyahimiza kupitia maandiko yake, alihimiza kuwalinda wazalishaji bidhaa wa ndani, dhidi ya ushindani kimataifa.

Ni matokeo ya sera, mikakati ya maendeleo, iliyoambatana na sheria, pia itikadi za kisiasa na hasa kati ya mwaka 1964 na 1985, mipango ya maendeleo ya miaka mitano tangu wakati huo ilitaka serikali kuwatambua wazalishaji wadogo.

Mantiki iliyokuwapo ni kutetea azma ya kujitegemea na kwamba watu hao wanapaswa kulindwa kimasoko, kwa sababu hawakuwa na uwezo wa kutosha kushindana, katika ngazi kama ya kanda na kimataifa,

Sura ya hilo, ilikuwa katika maudhui ya mipango ya miaka mitano ya kitaifa iliyokuwapo zama hizo na hadi kufikia mwishoni mwa miaka ya 1970, Mwalimu Nyerere alishaweka misingi ya mengi kiuchumi , katika eneo la viwanda.

### UFUFUAJI MASHAMBA

Hadi sasa katika serikali iliyopo madarakani, Rais Dk John Magufuli, inaendeleza fikra hizo katika mtazamo kukimbiza nchi katika uchumi wa viwanda, ni ufufuaji na uendelezaji zao la kibiashara mkonge.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amekuwa mstari wa mbele katika wajibu wake wa kutekeleza mikakati hiyo kuhimiza viwanda vinafufuka nchini na ili visimame, vinahitaji malighafi ambayo kwa kiasi kikubwa inatoka shambani, panapokuwapo uzalisaji mkubwa na mazao bora

Katika hilo kuna bidhaa mkonge, ambao Majaliwa, 'ameapa' serikali imedhamiria kulifufua na kuliendeleza zao hilo na viwanda nchini vintarajiwa kuboreka."

### MAJALIWA ZIARANI

Akihutubia mkutano wa wadau wa mkonge na viongozi wa serikali kutoka kada tofauti mjini hapa wiki iliyopita, Majaliwa, katika kauli anayoonyesha utayari wa kisiasa na kiuwekezaji, anakiri: "serikali imeingia kwa miguu miwili kulifufua zao hilo."

Anasema, Tanzania itakapofika kiwango cha juu cha uzalishaji mkonge, itafaidika na mbadala kuokoa fedha nyingi za kununua bidhaa zitokanazo na zao nje ya nchi.

> **"Zao hili lina faida kubwa na mambo haya lazima tuyaseme sisi wenye nia njema, tuwaambie wakulima wetu kwamba kilimo cha mkonge siyo cha matajiri tu.**



Shamba la mkonge lililoko mkoani Tanga.

Majaliwa anasema hadi sasa mkonge nchini unalimwa kwenye mikoa mitano; Tanga, Morogoro, Shinyanga, Mara na Kilimanjaro na kuna uwezekano wa mikoa zaidi kuzalisha.

Anataja manufaa ya mkonge ni kuinufaisha nchi kuokoa kati ya dola milioni 245 hadi milioni 250 (Sh. bilioni 563.5 hadi 575) zinazotumika kununua vifungashio nje ya nchi.

"Tukiokoa fedha hizi, zitabaki kuendeleza miradi mingine ya maendeleo nchini, ikiwamo ujenzi na uboreshaji wa miundombinu," anasema.

Waziri Mkuu anaeleza kushuka uzalishaji, tija na uwekezaji duni wa mkonge, umefikia hatua ya kukatisha tamaa uzalishaji, kukiwapo itikadi potofu kuwa ni zao la matajiri

"Napenda kuwaondoa uwoga. Ni wakati wa kuingia na kulima mkonge kwa sababu ardhi tunayo nzuri, wakulima wapo, uwekezaji upo, masoko yapo ambayo awali hayakutangazwa...mkakati wa pamoja ndio unahitajika kwa zao hili linalohitajika sana duniani," anasema.

Anatoa mfano wa gharama kwenye shamba la ukubwa ekari moja, mkulima anaweza kutumia Sh. 50,000 kuandaa trekta na Sh. 240,000 kununua jumla ya miche bora 1,600, malipo ya vibarua Sh. 120,000 na fedha za dharura zisizozidi Sh. 560,000.

Waziri Mkuu anafafanua, iwapo eneo litafanikiwa kuvunwa mkonge wa daraja analotaja '3L', bei yake kwa tani moja ni Sh. milioni nne, wakati ya daraja 'UG' ni Sh. milioni 3.5.

"Zao hili lina faida kubwa na mambo haya lazima tuyaseme sisi wenye nia njema, tuwaambie wakulima wetu kwamba kilimo cha mkonge siyo cha matajiri tu," anasema Majaliwa.

Majaliwa anasema, kwa sababu inachukua takribani miaka minne tangu ya maandalizi hadi kuvunwa, mkulima anaweza kulitumia kwa mipango ya muda mrefu, ikiwamo kugharamia masomo ya juu ya mtoto na miradi mingine ya maendeleo na uchumi wa familia.

Waziri Mkuu anahimiza uelimishaji huo unapaswa kufanywa na viongozi wa kada zote kutolewa kwa umma, kuanzia wizara, mikoa, wilaya hadi katika ngazi za msingi liliko jamii, zao lirejeshe kwenye heshima yake.

Takwimu zinaonyesha miaka iliyopita, Tanzania ilizalisha tani 200,000 za mkonge, ikashuka hadi tani 39,000 na sasa iko tani 35,000 na lengo la kimataifa ni kufikia tani 150,000 ifikapo 2025.

Anasema, azma hiyo itafikiwa kutokana na kuelekeza nguvu kwa wakulima wadogo, ufufuaji wa Bodi ya Mkonge, iliyowezesha mali zake ziliporwa na 'mafisadi' zikiwamo nyumba, viwanda na mashamba.

Pia, Waziri Mkuu anasema azma hiyo inahamasishwa na Rais Dk. Magufuli katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo (TARI) - Mlingano kilichopo Muheza, Tanga kwa kuwezesha ukarabati wa majengo yake, mitambo na ongezeko la vitalu vya miche bora kutoka ekri 10 kufikia 75.

Anasema halmashauri zilizopo maeneo kunakolimwa mkonge, kunapaswa kuanzisha vitalu vya miche vyenye ukubwa usiopungua ekari 10, ifikapo Aprili 30 mwaka huu.

### BODI YA MKONGE

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge, Saad Kambona, anasema ndani ya miezi 11 tangu kuteuliwa wameshatumia Sh.milioni 400 kukarabati jengo la ofisi, kurejesha nyumba 21 kati ya 32 'zilizoporwa' na sita zikiwa katika utaratibu wa ki-mahakama.

Pia, anasema bodi hiyo imelipa deni la kodi Sh. milioni 30 na gawiwo la serikali Sh.milioni 10, akibainisha katika kuwaunga mkono wakulima wadogo kwa maana pana iliyoko, ni kwamba walime kufikia kiwango cha wakulima wakubwa.

Kwa mujibu wa Saada, msimu uliopita wakulima wadogo walivuna tani 22638.6 katika mgawanyo, wakulima wakubwa wawili tofauti wana tani 4,622.53 na tani 8,277, huku wadogo walilima jumla tani 9,728.63.

### WATAALAMU WANENA

Mkurugenzi Mtendaji wa Chuo cha Utafiti Mlingano (TARI) Tanga, Dk, Catherine Senkoro, anasema kilimo cha mkonge kinapaswa kufanyika kwenye maeneo yaliyotathminiwa kitaaluma, ikiwamo kubaini hali ya udongo na hadi sasa TARI inazalisha miche bora ya mkonge jumla 120,000 katika maabara na lengo ni kufikia miche milioni tano kwa mwaka.

Mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Oscar Kibazohi, anasema matumizi ya mkonge nchini yapo chini kwa asilimia mbili tu ya mahitaji ya soko la ndani.

"Takribani asilimia 98 ya bidhaa zinazotokana na mkonge unaodumu kati ya miaka 15 hadi 19, huwa zinatupwa na hivyo kusababisha hasara kubwa," anasema Dk Kibazohi, anayeyaja bidhaa nyingine za mkonge ni uyoga, gesi baiolojia, kemikali, kilevi cha ethanol, chumvi limao, maji togwa yenye sukari

Mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) mkoani Morogoro, Dk. Cyriacus Ndyamukama, anaongeza kuwa mkonge unaweza kutengeneza chakula cha mifugo, hususani ng'ombe wa nyama, hasa wakati wa ukame.

### RC MARA

Mkuu wa Mkoa wa Mara , Adam Malima, anasema kutokana na ardhi iliyotumika kulima pamba mkoani kwake 'imechoka' sasa mkonge unaangaziwa kuwa fursa kwa wakulima wake.


Malima anasema wameshatenga ekari 20,000 kulimia mkonge kutoka 120,000 zinazotumika kwenye pamba.

Hata hivyo, bado kuna kilio cha walimaji wadogo kuhusu ugumu wa mitaji hasa kupitia mikopo ya benki 'wakikuka vichwa' wakulima na Waziri Mkuu Majaliwa, anaondoa hofu kuwapo mikopo hiyo kwa riba nafuu.

***• Mwandishi wa makala haya ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga. Anapatikana kwa simu: +255 754 691540.***

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Watanzania Uviko hakuna, je, mengine?






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**jkulangwa@yahoo.com**

WATANZANIA tuna haki na kila sababu ya kushukuru Mungu kwa anayotutendea, hasa katika suala la afya yetu, kutokana na gonjwa la UVIKO-19, ambalo sasa tunalisikia tu kwa mbaaali.

Maombi yetu ya siku tatu chini ya Rais wetu, John Pombe Magufuli mwaka jana, yalisababisha Uviko akimbie ghafla na kutuacha huru, baada ya kuhamanika kwa siku kadhaa.

Kwa sasa tumebaki kusikia wenzetu huko majuu na majirani, wakilia kutokana na ugonjwa huu, huku wakiendelea kupoteza ndugu zao na kila mara wakiziba nyuso kwa barakoa na kunawa kwa maji tiririka, sabuni na kujitenga hata kujifungia ndani.

Sisi utadhani tuko sayari tofauti kabisa walahi, hatuvai barakoa, hatujui sanitaiza wala kutengana na ndugu zetu, achilia mbali kujifungia ndani. Ndiyo kwanza, tunahimizwa kutoka kwenda kuchapa kazi, ili maisha yaendelee.

Kwa nguvu zake Jalali, Watanzania tumeamini kabisa hakuna Uviko, ingawa hivi sasa kuna 'gonjwa' linasumbuasumbua, la homa ya mapafu au Nyumonia (pneumonia), ambalo linajifanya kuja kama Uviko!

Limekuwa likitupora-pora ndugu zetu, lakini si kama kwa wenzetu ambao kwa kweli hali zao zinaendelea kuwa mbaya sana. La msingi sasa, ni kutafakari tu nini tufanye ili tuendelee kuchapa kazi, tusitengamane bali tutangamane.

Ipo haja pia ya kurudia kuvaa barakoa, kuhusiana na sanitaiza na kutengamana kwa muda, ili tuone Nyumonia naye akiondoka zake, sambamba na kumwomba Muumba kwa siku zingine tatu ili atuondolee balaa hili lingine.

Tusipofanya hivyo, kwa maana ya Mungu humsaidia ajisaidiaye, tutajikuta tunaingia katika wimbi lingine la maambukizi zaidi ya Nyumonia na kusambaratishwa, kama ilivyotaka kutokea enzi za mwenzake Uviko.

Tufanye hivyo tu, kwa sababu ni kuchukua hadhari kabla ya hatari, kwa sababu maradhi yote haya tunaletewa, hatuyaumbi wenyewe humu nchini. Si wote wanaopenda tulivyosalimika, la hasha!

Wapo wenye Uviko wanaotuonea inda wakitaka nasi tuhangaike nao, hivyo watatafuta kila njia watupenyezee hata Nyumonia kama hivi, ili tukose pa kutambia kuwa sisi ni salama na nchi yetu ni salama na watalii waje tu wajionee wakitakacho.

Kwa kuwa si rahisi kuwazuia watu hao kuingia nchini na kutuachia madudu yao, ni vema tukachukua hadhari hiyo ya kujikinga. Tusione aibu kutenga tena ndoo na sabuni nje ya malango ya makazi yetu kama awali, ili kila aingiye na kutoka ajitakase mikono.

Tusione soni kuvaa barakoa kwenye mikusanyiko ya watu kama ilivyokwa awali, hasa katika michezo, vyombo vya usafiri, mikutano na kadhalika, ikiwa ni kwa faida yetu, hata kama hakuna Uviko, lakini Nyumonia anazingua.

Tukatae kutangamana katika kipindi hiki ambacho tunadhani nyumonia inaingia kutushambulia pengine kwa njia tusioifahamu, tutengamane, ili kuepusha maambukizi haya, huku wakuu wetu wa afya, nao wakitafuta njia na mbinu nzuri za kutunusuru na hali hii, ambayo wengi sasa wameanza kuifananisha na Uviko.

Tukubaliane tu kuwa Uviko hakuna, ila nyumonia ipo, kwa sababu ilikuwapo na inaweza kuendelea kuwapo, pengine ufanano wa matatizo ya kushindwa kupumua, ndio unaotuchanganya. Lakini tuko salama.

Naamini Rais wetu anafuatilia kama alivyofuatilia na kutafakari na kuja na msimamo wa kumfukuzilia mbali Uviko, kwa maombi na nyungu. Tuendelee kubwia tangawizi, kunyonya malimao na kufanya chochote kinachoweza kutuepushia matatizo ya kupumua kwa shida, ili tuendelee kuijenga Tanzania. Alamsiki!

BIASHARA

# Mhariri Mkuu: COVID-19 iliniingiza darasani kujua nguvu ya teknolojia

## • Majibu ya ajira yalivyohamia TEHAMA

**Na Jenifer Gilla**



Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe.

"NILIKUWA sifahamu kama unaweza kufanya mikutano na watu wengi kutoka mataifa mbalimbali kwa wakati mmoja kwa kutumia mtandao, hii nimejifunza katika kipindi cha janga la mlipuko wa COVID-19," anasema Mhariri Mtendaji, wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, katika ufafanuzi WAKE alipohojiwa kuhusu changamoto na elimu aliyoipata katika kipindi hicho.

Ni sehemu ya mambo lukuki aliyojifunza bosi huyo, kutokana na 'mshikemshike' aliyopitia na kufanya akili yake kuchangamka zaidi ili kuendeleza kasi ya kiutendaji katika chombo hicho cha habari.

"Unapopitia changamoto ndipo akili inapochangamka, na mimi kupitia vigingi hivyo nimejifunza mambo mengi ambayo sikudhani kama yanawezekana," anasema, akitaja changamoto iliyomtambulisha duniani, ni Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari (TEHAMA).

Anaifafanua kuiwa inajumuisha kutolewa tamko la serikali kuepuka mikusanyiko, ili kujiepusha na maambukizi ya virusi vya corona ambavyo vinasababisha ugonjwa wa Covid-19, ambao huenea kwa kasi kwa njia ya hewa na kugusana.

Kwa mujibu wa Mhariri huyo, tamko hilo ambalo liliendа sambamba na kufungwa kwa mipaka kwa muda, lilimuumiza kichwa kutokana na ulazima wa kufanyika vikao vya kila siku katika kitengo chake.

"Kazi yetu hapa inahitaji vikao vya kila siku, ili kupangiana majukumu na waandishi wa habari pamoja na wahariri wenzangu, zile siku za mwanzo ambazo hatukufanya vikao niliona kabisa utendajikazi hauendi sawa.

Ndipo kupitia kwa vyombo vya habari vingine nikajifunza teknolojia hii, tukawa tunafanya vikao kwa njia ya mtandao (zoom meeting) kila mtu akiwa eneo lake na mambo yakaenda sawa," anasema.

Pia, baadhi ya waandishi walilazimika kufanyia kazi wakiwa nyumbani ili kupeana nafasi ofisini na kwa njia hiyo mikutano ya kimtandao ilisaidia kupeana majukumu.

Kuzuiwa kwa safari za nje na ndani ya nchi, ni sababu nyingine iliyomtambulisha kwenye ulimwengu wa mikutano ya njia ya mtandao bosi huyo ambaye alizoea kufanya hivyo katika kutimiza majukumu yake.

Anasema, tangu hapo alianza kutumia mtandao wa 'zoom' na mingineyo kufanya mikutano na wadau wa nje ya nchi na mambo yakaenda sawa.

"Juzi tu hapa tumetoka kusaini mkataba na wadau ambao hatujawahi kuonana zaidi ya mikutano ya 'zoom' kwa sababu mataifa mengine, bado ugonjwa huo upo hivyo sio salama kutoka nje ya nchi zao," anasema.

Bandawe anaisifia teknolojia hiyo kuwa muhimu hasa katika vyombo vya habari, kwa kurahisisha kazi na kubana matumizi ya fedha.

"Vikao vya kiutendaji vya wakuu wa idara pia ofisini vilisimama kipindi cha corona, lakini kupitia teknolojia ya mtandao, mambo yalienda kama kawaida kwa kupeana taarifa na majukumu.

"Natamani hata waandishi wa habari wafundishwe teknolojia hii ili iwasaidie katika utafutaji wao wa habari kama vile, kuhudhuria mikutano ya kimataifa na kuhoji watu, hii itasaidia wakati mwingine kuokoa muda na pesa," anasema.

Licha ya teknolojia hii kurahisisha utendaji kazi wake, anakiri kuwa imemuweka karibu na ndugu na jamaa zake walipo nje ya nchi kwa kuwa tofauti na zamani sasa wanawasiliana na kuonana tabasamu zao.

Kinachomfurahisha zaidi ni kuwaona ndugu zake walioko nchi tofauti kwa wakati mmoja na wakaonana na kufurahi kama vile wamekaa kibarazani.

Pia, anatoa ushuhuda jinsi ambavyo teknolojia hii imempa nafasi ya kuhudhuria tukio muhimu la kumuaga kaka yake.

Anasema: "Kupitia mtandao wa zoom tulifanikiwa kumuaga kaka yetu mpenzi ambaye alikuwa katika dakika za mwisho za kuiga dunia kutokana na maradhi ya moyo yaliyokuwa yanamsumbua kwa muda mrefu yaliyoambatana na maambukizi ya virusi vya corona."

Ingawa hawakupata nafasi ya kumzika kwa kuwa alifariki dunia akiwa nchini Marekani na kuzikwa huko, Bandawe anasema alifarijika kumuaga kaka yake kabla hajafariki.

### ASHUHUDIA CHANGAMOTO

Katika nafazi yake ya kuongoza gazeti, Bandawe anakiri kupitia changamoto nyingine nyingi, alizopambana nazo kuhakikisha kazi zinasonga mbele.

Kutokana na janga la mlipuko wa corona, kampuni nyingi ziliyumba kiuchumi hivyo kulazimika kupunguza idadi ya wafanyakazi.

Kampuni ya The Guardian, nayo ililazimika kufanya mchakato huo, ili kuinusuru isiendelee kujiendesha kwa hasara.

Akiwa mmoja wa wanaofanya uamuzi mkuu, Bandawe anasimulia ilivyokuwa vigumu kuamua, akitamka: "Kilikuwa moja ya kipindi kigumu nilichopitia katika utendaji kazi wangu.

"Nilikuwa sioni wa kumpunguza kwa sababu ofisi, ilikuwa na wafanyakazi wachache kwa kuwa tulishapunguza huko nyuma, pili ni watu ambao nimewazoea na kila mmoja anafanya kazi wa weledi.

"Kama kiongozi kwa kushirikiana na viongozi wengine ilibidi tufanye uamuzi mgumu, lakini ilikuwa kuwapumzisha kwa muda wa miezi mitatu kisha warudi tena na ninashukuru walirudi," anasema.

Kupunguzwa mishahara kwa wafanyakazi kilikuwa ni kigingi kingine kwa bosi huyo, anaeleza kukosa amani kila alipokuwa akiona nyuso za wafanyakazi wake zenye ishara ya kukata tamaa, lakini hakuwa na jinsi.

"Ulikuwa uamuzi mgumu, ilikuwa ni lazima tufanye hivyo ili kunusuru kupunguza wafanyakazi wengi zaidi, ilibidi tupunguze kati ya asilimia 20 kwa wenye mishahara mikubwa na asilimia 10 wenye mishahara midogo kwa miezi mitatu.

"Hapa nilijifunza pia kuwafundisha wafanyakazi wenzangu kuikubali hali hii mapema kwa kuwa hakukuwa na namna nyingine na ilifanya kazi," anaelezea kwa ujasiri.

Hofu ya kupata maambukizi ya COVID-19 iliyoonekana waziwazi kwa wafanyakazi wake ilimnyima raha kiongozi huyo kwa kuwa aliona wazi kuwa ingezorotesha utendaji kazi.

Kwa mujibu wa Bandawe kutokana na uhalisia wa kazi yao, waandishi walihitajika kutoka kwenda kutafuta habari mitaani hivyo afya zao zilikuwa hatarini.

"Ingawa walikuwa wanachukua tahadhari zote muhimu, lakini kuna nyingine zilikuwa hazieрukiki kama vile misongamano, kugusana, kwa hiyo hofu ilikuwa ni kubwa hivyo tulifanya kazi kubwa ya kuhakikisha tunapambana na hofu," anasema.

Pamoja na changamoto zote alizopitia, Mhariri Mtendaji huyo anamshukuru Mungu kwa kuwa alivuka changamoto hizo salama na hakuna mtu aliyepata maambukizi katika ofisi yake.

Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa inayoshughulika na Wanawake (UN WOMEN) inaonyesha kuongezeka kwa maambukizi ugonjwa wa COVID-19 hadi Machi 2020 wanawake wameingia kwenye kinachoitwa 'kazi ziziso na malipo' kutokana na uhalisia wa familia zao, tofauti na wanaume.

Kazi hizo ni kama kulea watoto. Inatajwa jumla ya wanafunzi bilioni 1.5 duniani walikuwa nyumbani kupisha maambukizi, kulea wazee, kuuguza waume zao, na kuhudumia watu wao wa karibu hali iliyowarudisha nyuma kimaendeleo na wengine kulazimika kuacha kazi.

Machi 16, 2020 Tanzania ilitangaza mgonjwa wake wa kwanza wa virusi vya Covid19 na Machi 17, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alitangaza kufunga shule zote kuanzia za awali hadi vyuo vikuu.

Vilevile, alizuia mikusanyiko mikubwa ya ndani na nje ya nchi na safari za kimataifa zisizo na ulazima, kuzuia kuenea maambukizi ya ugonjwa Covid-19 nchini.





# Wanawake waambiwa tiba ya udumavu ni kunyonyesha

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

WANAWAKE wametakiwa kuwanyonyesha watoto wao katika kipindi cha miezi sita bila kuwalisha chochote ili kuwalinda na magonjwa na kuwaepusha na udumavu, lakini kuendelea kunyonyesha kwa miaka miwili kama inavyoshauriwa kitaalamu ili kuwaepusha na udumavu.

Ushauri huo ulitolewa na Katibu wa Jumuiya ya Wanawake wa UWT, wilayani Bahi Lucia Sulle, wakati alipokuwa akizungumza na kinamama waliojifungua katika kituo cha afya cha kata ya Chifutuka wilayani humo.

Akizungumza na kina mama hao kwenye maadhimisho ya miaka 44 ya kuzaliwa kwa CCM, ambayo pia yaliambatana na utoaji wa misaada mbalimbali kwa ajili ya wagonjwa waliolazwa na kufanya usafi katika kituo hicho.

Katibu huyo alisema kuwa watoto wanapaswa kunyonyeshwa kwa muda unaostahili ili waweze kuwa na afya timamu ya kimwili na kiakili.

Alisema kuwa pamoja na shughuli mbalimbali wanazozifanya zikiwamo za kilimo, ufugaji na ujasiriamali, hakuna sababu ya kuwaachisha watoto wao kunyonya kabla ya wakati.

"Hivyo ninawaomba wanawake na akina mama wenye watoto wezangu hakikisheni mnawanyonyesha watoto wenu kwa muda unaostahili, na kamwe msidanganywe na shughuli mlizonazo na mkasahau kuwanyonyesha na mkawaachisha kabla ya muda wao, mnaweza kuwasababishia maradhi yasiyotarajiwa"alisema.

Mwenyekiti wa jumuiya hiyo ya wanawake wilayani Bahi Stella Boma, akizungumza katika sherehe ya maadhimisho ya miaka 44 ya CCM aliwataka kufanya kazi.

Alisema ili kujiinua kiuchumi wanahitajika kufanya kazi kwa bidii na kuachama mazoea ambayo siku zote yamekuwa yakisababisha kuleta umasikini miogoni mwa familia.

Aliwaomba wanawake wa kijiji hicho kuwa mstari wa mbele kuwapeleka watoto shule kwa wanaotakiwa kuanza darasa la kwanza na wale waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza.

Alisema kuwa kwenye familia mama ndiye mlezi mkubwa hivyo ni mategemeo yake kina mama wataungana na serikali kuhakikisha hakuna mtoto anayestahili kwenda shule anayebaki nyumbani bila sababu ya kujitosheleza.

# TAKUKURU yaibua mkakati wa mihadhara kuibua rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma imeanzisha utaratibu wa kuwapa nafasi wananchi wanaoshindwa kwenda katika ofisi zao kuripoti rushwa, kutoa malalamiko yao kwenye mihadhara.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa TAKUKURU Dodoma, Sosthenes Kibwengo, wakati akielezea namna klabu za kupinga vitendo dhidi ya rushwa zilizopo jijini hapa zinavyofanya kazi.

Aliwataka wakazi wa Dodoma kutumia fursa hiyo kujitokeza kwa wingi kutoa kero zao kwa taasisi hiyo ambazo nao watazifanyia uchunguzi kujua kama zina ukweli.

Mbali na hilo Kibwengo alisema taasisi hiyo itaendelea na utaratibu wa kukutana na wakazi wa Dodoma katika maeneo tofauti kwa ajili ya kusikiliza kero mbalimbali za rushwa.

Alisema hatua hiyo ni moja ya utekelezaji wa majukumu ya TAKUKURU ili kuhakikisha wananchi wanapata haki zao ya msingi si kwa kuzinunua.

Alisema taasisi imetumia mbinu mbalimbali kuhamasisha jamii katika mapambano dhidi ya rushwa ambayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuelimisha wananchi kuhusu suala zima la kupiga vita rushwa.

Aidha,alisema mwaka huu wamejipanga kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya kupambana na rushwa,kwa kukitumia mikutano na maonyesho ya hadhara kwa jamii ili waweze kupata elimu na kufikia mabadiliko.

Aidha, Kibwengo alisema TAKUKURU itaendelea kutoa elimu ya kupinga rushwa kwa jamii, ili kuhakikisha kila mmoja anatambua haki yake ya msingi katika eneo lake.

Kibwengo alisema taasisi hiyo imetenga muda wa kutembelea maeneo mbalimbali jijini hapa kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu namna ya kupinga rushwa katika sehemu za kazi, vyuoni na shuleni.

"Matokeo ya jitihada ya elimu tunayotoa tunaiona inavyoifikia jamii ipasavyo, tunapata taarifa za viashiria vya rushwa katika ofisi zetu, nasi tunazifanyia kazi," alisema Kibwengo.

Kutokana na hilo aliitaka jamii kuendelea kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU wa kutoa taarifa pale wanapoona kuna viashiria vya rushwa ili wazifanyie uchunguzi kubaini ukweli.

Alisema mapambano dhidi ya rushwa ni ya kila mmoja, hivyo wananchi wanapaswa kuendelea kutoa taarifa pale wanapoona sehemu kuna viashiria vya rushwa.



Mwenyekiti wa Taifa wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Gaudensia Kabaka, akizungumza na viongozi wa ngazi mbalimbali wa Makao Makuu ya CCM, jijini Dodoma jana, ikiwa sehemu ya maadhimisho ya miaka 44 ya chama hicho. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wavamizi madaraja waamriwa kuondoka

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, amewataka wafanyabiashara ndogo au wamachinga, kuacha kufanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi yakiwamo madaraja ya wanaotembea kwa miguu.

Onyo hilo alilitoa juzi wakati alipokuwa akiwaelimisha wafanyabiashara hao ambao baadhi yao wamepanga bidhaa katika madaraja yanayotumiwa na wanaotembea kwa miguu yaliyojengwa na halmashauri ya jiji.

Alisema baadhi ya madaraja hayo yaliyopo ndani ya jiji hivi sasa yamevamiwa na wamachinga na kujazwa bidhaa bila kujali maana halisi ya miundombinu hiyo iliyokusudiwa na mipango miji.

Alisema kuwa watembea kwa miguu wanapita kwa shida na kusababisha adha kwa vile biashara zimetapakaa ovyo na kusababisha wanaotumia madaraja hayo kukosa maeneo ya kukanyaga.

Pia alisema hata upangaji wa bidhaa hizo kwenye madaraja hayo unaweza kuhatarisha maisha ya wafanyabishara wenyewe na kwa wateja wanayo yatumia.

"Hivyo niombe tuheshimu matumizi ya madaraja haya ambayo serikali imeyajenga ili kuwahudumia wanaotembea kwa salama kwa maana hiyo ninahitaji yawe wazi na sivyo vinginevyo"alisema

Aidha aliwataka mamalishe ndani ya masoko kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya kwa kuweka vyombo vya kunawa na sabuni ili kujikinga na magonjwa mbalimbali ya mlipuko.

Akizungumza na mama lishe wa soko kuu la majengo jijini Dodoma, alisema kuwa wanatakiwa kuchukua tahadhali ya magonjwa ya maambukizi, hivyo ni muhimu wafanye shughuli zao katika mazingira usafi.

# Wafugaji walilia maeneo ya kufugia

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

WAFUGAJI wa Kijiji cha Kimondo kilichoko Kata ya Igoma Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali iwapatie maeneo ya kuchungia mifugo yao kwa madai kuwa waliyokuwa wanayatumia awali yalichukuliwa na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) na kuyafanya kuwa sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Kitulo.

Walitoa ombi hilo juzi, wakati walipokuwa wanakabidhiwa dawa za kuogesha mifugo zilizotolewa bure na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenye josho la kijiji hicho, ikiwa ni mikakati ya serikali kuwasaidia wananchi kuboresha mifugo yao.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Subi Njate, alisema kijiji hicho kwa sasa hakina eneo lolote la kuchungia na hivyo wafugaji wanalazimika kuchungia kwenye maeneo madogo yaliyomo pembezoni mwa mashamba.

Alisema hali hiyo inasababisha migogoro ya mara kwa mara na wakulima kutokana na mifugo kula mazao ya wakulima na kwamba hawawezi tena kuchungia kwenye eneo lao la awali kwa sababu sheria zinazuia.

"Tunamuomba Rais Magufuli kama anatusikia atusaidie tupate maeneo ya kuchungia mifugo yetu maana tunapata shida sana, sasa hivi tunapishana sana na wakulima kwenye mashamba yao," alisema Njate.

Aliishukuru Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuwasaidia dawa hizo za kuogesha mifugo kwa maelezo kuwa zina faida kubwa kwa wafugaji ikiwemo kuboresha mifugo na kuongeza tija.

Baadhi ya wafugaji wa Kijiji hicho, walisema tangu Serikali ilipoanza kuwapatia dawa hizo wamepata manufaa makubwa kutokana na mifugo yao kuwa na afya njema na kuongeza kasi ya kuzaliana tofauti na ilivyokuwa awali.

Mmoja wa wafugaji hao, Modestus Shungu, alisema awali kabla ya Serikali kuanza kuwapatia dawa hizo walikuwa wanalazimika kuchangishana wao wenyewe na kwamba ilikuwa dawa zikiisha na wao wanatelekeza josho.

Aliiomba Serikali iendelee kuwasaidia dawa hizo ili waendelee kunufaika na shughuli yao ya ufugaji ambayo ni miongoni mwa shughuli zinazowaingizia kipato kikubwa.

Naye, Kenedy Jafari alisema kabla hawajaanza kuogesha mifugo yao ilikuwa inakumbwa na magonjwa mbalimbali ambayo yalikuwa yanasababisha mifugo hiyo kufa.

"Hata maziwa tulikuwa tunapata kidogo, lakini tangu tulipoanza kuogesha dawa hizi ambazo tunapewa na Serikali mifugo yetu inazaliana sana na maziwa tunapata mengi sana, tunaomba Serikali iendelee kutusaidia," alisema Jafari.

Akiwakabidhi wafugaji wa Kijiji hicho dawa hizo kwa niaba ya Wizara ya Mifugo, Daktari wa Mifugo wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Samora Mshang'a, alisema Mkoa wa Mbeya una zaidi ya mifugo 500,000 na kwamba wanaendelea kuogesha kwa awamu.

Alisema Serikali imetoa lita 350 kwa ajili ya majosho yote yaliyoko ndani ya Mkoa huo na kwamba dawa hizo zitatosha kuogesha mifugo isiyopungua 40,000.

Alisema dawa hiyo itatosha kuogesha mifugo hiyo kwa muda wa miezi sita kuanzia sasa na akawataka wafugaji hao kuchangamkia fursa hiyo ya kuogesha mifugo hiyo.



Baadhi ya vijana wa Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, wakijitafutia riziki kwa kusafirisha ndizi kwa kutumia pikipiki kutoka kwenye mashamba ya wakulima yaliyopo kijiji cha Kiimo kupeleka katika Soko la Kiwira wilayani humo juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**.

## Wakulima wadai mvua kuharibu mazao yao

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

WAKULIMA wa viazi mviringo katika Kata ya Ilungu Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamesema mvua inayoendelea kunyesha mkoani hapo, imesababisha mazao yao kuanza kuharibika kwa kuungua hali ambayo inatishia mavuno kupungua.

Wakizungumza na Nipashe juzi wananchi hao walisema hali hiyo imesababisha hata gharama za uzalishaji kuongezeka kutokana na dawa za kuzuia ukungu kuuzwa bei kubwa, huku baadhi wakidai kuwa wanashindwa kumudu gharama.

Mmoja wa wakulima hao, Joseph Sote, alisema kutokana na hali hiyo ya mvua kubwa, wanalazimika kuweka mbolea hata mara mbili kutokana na mvua hiyo kusomba kila wakishaweka na hivyo gharama kuzidi kuongezeka.

"Huku kwetu viazi vinalipa zaidi wakati wa kiangazi kwa sababu huwa hatutumii gharama kubwa kwenye uzalishaji, sasa hivi kama unavyoona viazi vimeungua mno, sasa hivi hata mbolea tunazotumia ni nyingi kuliko inavyokuwa kiangazi," alisema Sote.

Naye Vumilia Mshombe, alisema pamoja na gharama hizo kuwa kubwa lakini bei za kuuzia viazi hivyo huwa zinakuwa chini kiasi kwamba hazisaidii kurejesha gharama za uzalishaji wanazotumia.

Alisema wanunuzi wa viazi hivyo huwa wanaenda na bei ambazo wanajipangia wenyewe na hivyo kuzidi kuwadidimiza kiuchumi wakulima hao.

# Mbeya yaja na mkakati ujenzi wa mabweni

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

SERIKALI mkoani Mbeya imesema itahakikisha kufikia mwaka 2025 nusu ya Shule za Sekondari za Jiji la Mbeya zitakuwa zimejengewa mabweni na madarasa, ili wanafunzi wote hasa wa kike wakae shuleni ili kuboresha kiwango cha elimu na kuwaepusha na mimba za utotoni.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, wakati wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ilipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ya maji, afya na elimu.

Akizungumza katika Shule ya Sekondari Wigamba iliyopo katika Kata ya Isanga jijini hapa ambayo ilikuwa inakabiliwa na uhaba wa vyumba viwili vya madarasa, Chalamila alisema wanapotoka nyumbani kwenda shuleni kila siku huwa wanatumia muda mwingi kufanya vitu visivyofaa.

Alisema wakati wanajiandaa kujenga mabweni hayo, sasa hivi Serikali inakusudia kuhakikisha wanafunzi wote wanakula chakula cha mchana shuleni kwa maelezo kuwa njaa huwa inawafanya wanafunzi wasifuatilie masomo.

"Lakini pia tunatakiwa kuwaepusha vijana wetu na vishawishi, takwimu za maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (HIV) kwa vijana zinatisha, takwimu zinaonyesha kuwa vijana wanaopata zaidi maambukizi ni wenye umri kati ya miaka 15 mpaka 24 ambao wengi ndio hawa wanafunzi," alisema Chalamila.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa kwa mwaka vijana wa umri huo huwa wanaopata maambukizi ya VVU ni zaidi ya 72,000 na kwamba takwimu zinaonyesha kuwa maambukizi katika Mkoa huo yamefikia asilimia 9.3.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya ambaye ndiye aliyeiongoza kamati hiyo ya siasa, aliipongeza Serikali ya Mkoa huo kwa maono ya kujenga mabweni akidai kuwa utaratibu huo utasaidia kuwaepusha wanafunzi na vishawishi.

Aliwataka wananchi wa Mkoa huo kushirikiana na Serikali katika kuboresha miundombinu ya elimu ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, vyoo, maabara na mabweni ili wanafunzi wasome katika mazingira mazuri.

"Ni kweli yawezekana watoto wetu wa kike wanashawishiwa na wanaume kwa kupewa mihogo na chips wanapokuwa na njaa, sasa ni vizuri tujitahidi huu utaratibu wa chakula cha mchana utekelezwe ili kuwapunguzia vijana vishawishi," alisema Mwakasole.

Aliwataka wanafunzi kusoma kwa bidii na kuepuka kushiriki mapenzi wakiwa bado na umri mdogo kwa maelezo kuwa wanaweza wakakatisha masomo yao kwa kupata mimba na magonjwa ya zinaa ambayo yanaweza yakagharimu maisha yao.

Aidha, Mwakasole alisema waliridhishwa na ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na osifi moja katika shule ya Sekondari Wigamba huku akiutaka uongozi wa Kata ya Isanga kuboresha vyoo vya wanafunzi ili kuwaepusha na magonjwa ya mlipuko.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Amede Ng'wanidako, alisema wanafunzi 60 wa kidato cha kwanza walioukwa wamechaguliwa kujiunga na shule hiyo walichelewa kuanza masomo kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.



# Wanasheria wahimizwa kupambana udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka wanasheria kutumia elimu waliyonayo kuendeleza mapambano ya vitendo vya udhalilishaji na kuelimisha jamii kuhusu madhara ya vitendo vya rushwa.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na viongozi wa Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), walipofika ofisini kwake Vuga kujitambulisha.

Alisema vitendo hivyo vya udhalilishaji vimekuwa vikiwakuta zaidi watoto hivyo umefika wakati kila mtu aone anawajibika kuunga mkono juhudi za serikali kutokomeza vitendo hivyo.


Alisema katika mapambano hayo, serikali imeshaanza kuzipitia sheria zote zinazohusu vitendo vya udhalilishaji ili iwe rahisi kuendesha kesi za aina hiyo na aliitaka jamii kuacha mzaha katika kutoa ushahidi kwenye kesi hizo.

Aliipongeza jumuiya hiyo kwa kazi wanazoendelea kufanya hasa kwa kuwaelimisha wanawake kuhusu uelewa wa sheria ili kujua haki zao.

Aliwataka wanasheria hao kutokata tamaa na kutovunjika moyo katika kazi wanazofanya na badala yake waungane na kasi ya serikali yenye lengo la kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Jumuiya hiyo, Jamila Mahmoud Juma, alisema jumuiya hiyo imefanikiwa kutoa elimu kwa jamii hasa vijijini na kueleza kuwa wamekutana na matatizo mbali mbali ikiwamo uelewa mdogo wa jamii kuhusu udhalilishaji na elimu ya rushwa.

Naye Mwenyekiti wa ZAFELA Zanzibar, Safia Hija, alisema jumuiya yao kisheria imepata mafanikio makubwa kwa kuwasaidia wanawake mahakamani ili kupata haki zao.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Zanzibar, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mussa Haji Ali (kulia), akikabidhiwa vitendea kazi wakati wa makabidhiano ya ofisi na aliyekuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu, Salum Maulid Salum, katika hafla iliyofanyika Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU.**

# Sheria ya Maadili Zanzibar kurekebishwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inakusudia kuwasilisha marekebisho ya sheria ya maadili ya viongozi wa umma ambapo watendaji wanaosimamia fedha wakiwamo wahasibu wataingizwa.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utawala Bora na Utumishi wa Umma, Haroun Ali Suleiman, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mazizini Mjini Unguja.

Alisema kada ya wahasibu na wafanyakazi wengine wanaosimamia fedha ni muhimu sana ambao wanatakiwa kutaja mali zao na kujua njia walizotumia kuzipata.

Alieleza kuwa serikali inakusudia kufanya marekebisho hayo baada ya kutokea kasoro mbali mbali za kiutendaji kwa baadhi ya watendaji wakiwamo wahasibu.

Alisema hatua hiyo imesababisha serikali iwasimamishe kazi wahasibu 80 kupisha uchunguzi zaidi kwa tuhuma mbali mbali ikiwemo kuchezea mfumo wa fedha na kutoa risiti za mkononi kwa lengo la kuikosesha serikali mapato.

"Uchunguzi kuhusu wahasibu 80 waliosimamishwa kazi unaendelea ambapo watakaobainika hawahusiki na tuhuma hizo wataachiwa na kurudi kazini....wale watakaobainika kuitia hasara serikali hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao," alisema.

# Katibu Mkuu aomba ushirikiano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mussa Haji Ali, amesema kuna umuhimu kwa watendaji wa ofisi hiyo kushirikiana ili iwe rahisi kwao kutekeleza majukumu yao.

Aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar, wakati wa makabidhiano ya ofisi kati yake na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Salum Maulid Salum.

Alisema anamatarajio makubwa ya kuwapo kwa ushirikiano kati yake na watendaji wa ofisi hiyo ambako kutasaidia kuimarisha utendaji wa kazi hasa kwa umuhimu wa ofisi hiyo sanjari na kwenda na kasi ya maendeleo iliyokusudiwa.

Aidha, alisema mbali ya umuhimu wa ushirikiano, suala la mawasiliano miongoni mwa viongozi na watendaji wa ofisi hiyo ni jambo la muhimu na litasaidia katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Naye aliyekuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Salum Maulid Salum, alimpongeza Katibu Mkuu huyo mpya kwa kushika wadhifa huo na kueleza kuwa kutokana na uchapakazi wake ana matumaini makubwa kwamba atatekeleza vyema majukumu yake hayo mapya.

Aidha, alitoa pongezi na shukrani kwa watendaji wote kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika ofisi hiyo na kusisitiza kwamba mafanikio hayo yametokana na ushirikiano, umoja na mshikamano kati yao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**WACHIMBAJI BORA WA VISIMA VYA KISASA TANZANIA:**

Tunachimba Visima vya Kisasa Virefu na Vifupi katika Mikoa yote Tanzania. Tunatumia Mashine Bora na za kisasa za kuchimbia Visima katika Ardhi ya Tanzania. Gharama zetu ni nafuu. TUPIGIE SIMU: 0657 990015 / 0759 848155 / 0788 409536

**TUNAUZA SHELL 5 (PETROL STATIONS) VITUO VYA MAFUTA.**

VIBALI VYOTE VIMEKAMILIKA. JE? UNATAKA KUNUNUA SHELL. WASILIANA NA TANLANDS REAL ESTATE: SIMU: 0759 848 155

Uza,
Chenye Thamani Kubwa
Kwa Kutangaza Nasi Kwa
Bei Poa
Tupigie 0782253676

## REQUESTING FOR COPY RIGHTS

**Annestella K. Mutoka** is requesting the managing directors of Ben and Company ltd,the copyright for the following books.

1. Jifunze kwa picha 1,wanyama wa nyumbani (1993)
2. Jifunze kwa picha 2,wanyama wa mwituni (19930
3. Kifaru (2015)

The letter should be addressed to A. Mutoka P.O.BOX 66769, Dar es salaam

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CMG INVESTMENTS LTD** wanatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MERCEDES BENZ** yenye namba za usajili **T 477 DTQ** chasis namba **WDB2110612A172573** engine namba **11291331429991**,yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi **DSM/PHQ/RB/67224/2021**

## KUPOTEA KWA VYETI



**KALISTA KALISTUS NYIMBO** mwenye picha apo juu amepotelewa na Cheti Cha kumaliza elimu ya sekondari form four mwaka **2008** chenye namba ya usajili

**P.2517-0142/ACSEE** alichopewa na shule ya **Alfagems.**
Kwa yoyote atakaye kiona atoe taarifa kituo chochote Cha polisi.


**RB no; MORO/MORO/RB/68520/2021.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ISACK OMSHUMBA BARNABA** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4645.0021** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **ALLIANCE BOYS** mwaka 2014 , yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.Polisi taarifa **KIG/KIG/RB/697151/2020**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ISSA RAMADHANI GWAU** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo, cha kidato cha nne chenye index namba **S1549-0091** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **ENGUTOTO** mwaka **2010**,Pamoja na **CERTIFICATE** na cheti cha **DIPLOMA COLLEGE OF BUSINESS EDUCATION** chenye index namba **OD1003IF/D3 2013** mwaka **2015.**
Yeyote atakayevikota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa KAH/RB/7166/2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA (MCA/84)**

**MAHAKAMA YA MWANZO YA (W)IRINGA MJINI WILAYA YA IRINGA**

**SHAURI LA NDOA 9/2021**

**MDAI: GRACE D/O NYARARA**

**MDAIWA :ISACK S/O AKELO**

KWAKUWA MDAI AMELETA MADAI YAKE YA KUACHANA NA MDAIWA ,KWAHIYO UNAHITAJIKA KUHUDHURIA BINAFSI KATIKA TAREHE 15.2.2021 SAA 2.30 ASUBUHI KWA KUJIBU DAI. KWAKUWA SIKU HIYO YA KUKATWA SHAURI HILO NI LAZIMA KULETA MASHAHIDI WENU NA HATI ZOTE ZINAZOHUSU SHAURI HILO KWA AJILI YA KUJITETEA KATIKA SHAURI HILO.

USIPOFIKA SHAURI LITASIKILIZWA UPANDE MMOJA.

**HATI HII IMETOLEWA LEO 2/2/2021**

**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI.**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NA 97 YA MWAKA 2020**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**NOAH PATRICK NKINDIKWA**
**WAOMBAJI RHODA WILLIAM BONGOHE NA MATHIAS PATRICK NKINDIKWA**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 17TH mwezi February 2021
Imewasilishwa Dar es salaam leo tarehe 03 mwezi February 2021

NAKALA KWA
NAIBU MSAJILI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**katika Mahakama ya Mwanzo CHAMWINO MJINI Wilaya ya DODOMA MJINI**

**MADAI NAMBARI 13/2020**

**MDAI KAMO MICROFINANCE LTD**

**MDAIWA MICHAEL LUHEDEKA LUKANDA**

**KWA MICHAEL LUHEDEKA LUKANDA**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba**

**MADAI YA ZUIO**

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMANNE tarehe 09/2/2021 saa 8:00 asubuhi/Alasiri kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi *wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia Na kama *hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikidhibitisha kama *umepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kwa kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo 04/02/2021.

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ROBERT K MKONGWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 252 BMB.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.Taarifa ya polisi **MBE/MBE/RB/67647/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Mkumbwa Iddi Ramadhani** Mkazi wa Ndala Mkoani Shinyanga anatangaza kupoteza kadi yake ya pikipiki aina Honda **CT 110** trail yenye namba za usajili **MC 451AAG**,Injini namba **JDOE1053201** na cheses namba **JDOI1048712.** Yoyote atakayekuwa ameiokota aiwasilishe katika kituo cha polisi Shinyanga.
Taarifa imetolewa kituo cha polisi kwa namba ya malipo **991082316729**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NIKOBIBA ALBERT KIGADYE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 122 DNC TOYOTA CROWN.** Chassis namba **GRS1805013242.** Engine namba **4GR0064899.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: CONTROL NUMBER **9910819749609**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Sisi **AJ RECOVERIES LTD** kwa idhini tuliyopewa na **LETSHEGO BANK (T) LIMITED– TAWI LA MANZESE,** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wa benki ya **LETSHEGO** ili kufidia deni lake;

| S/NO | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | MAHALI ILIPO | SIKU NA TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | VALENCY CHARLES KALANGA | NYUMBA IMEZUNGUSHIWA UZIO. PLOT 726 BLOCK "C" MADALE, MANISPAA YA KINONDONI. | MTAA WA MADALE KATA YA WAZO. ENEO LA MITIKINI | JUMANNE 20/02/2021 SAA 06:00 MCHANA. |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mnunuzi atalipia asilimia 25% ya bei ambayo imefikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki anatakiwa kumaliza ndani ya siku kumi na nne(14), endapo atashindwa kumalizia salio lililobaki mnada utarudiwa upya na fedha iliyolipwa haitarudishwa. Ukaguzi wa dhamana ni kwa kuwasiliana na dalali au Tawi la benki Husika siku yoyote muda wa kazi.
2. Gharama za kubadilisha umiliki wa dhamana ni ya Mnunuzi.
3. Dhamana itauzwa jinsi ilivyo.

**AJ RECOVERIES LIMITEDIREG:141077236IShekilango sokoniIUbungo I P. O. Box 1056 I Dar Es Salaam ITanzania, (Mobile) +255 686153126 : (Mobile) +255 746 336875**

## NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Sisi **Dabri Auction Mart Company Limited** kwa idhini tuliyopewa na **Benki ya Letshego** na mamlaka tulionayo kisheria tunatoa notisi ya siku 14 kuanzia siku ya tangazo hili kwa mdaiwa na mdhamini walipe deni lao lote kinyume na hapo tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana zao tajwa kama ilivyoorodheshwa hapa chini:

| S/N | JINA LA MKOPAJI | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | ENEO ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | HATI NAMBA 110128 KIWANJA NAMBA 249 KITALU NAMBA 6 | KIBADA,MANISPAA YA TEMEKE | TAREHE 22/02/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 2. | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | HATI NAMBA 121999 KIWANJA NAMBA 135 KITALU NAMBA 32 | BUYUNI,MANISPAA YA ILALA | TAREHE 22/02/2021 SAA 9:00 ALASIRI |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi atalazimika kulipia 25% ya bei iliyofikiwa kwenye mnada na salio la 75% litalipwa ndani ya siku 14 tangu siku ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipia salio ndani ya siku 14, atakua amepoteza haki yake ya malipo ya 25% na dhamana itauzwa tena.
3. Gharama zote kuhusu kubadilisha jina na umiliki wa dhamana zitakua juu ya mnunuzi.

**Kwa maelezo zaidi fika kwenye ofisi zetu zilizopo Mwananyamala au wasiliana nasi kwa namba za simu 0713401175 na 0657507050**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Tanzania, Burundi hazimo orodha kupatiwa chanjo ya Covid-19

**New York, MAREKANI**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limetangaza mpango wa muda kuhusu nchi zitakazopatiwa chanjo ya corona barani Afrika, mwaka huu, Tanzania na Burundi hazimo kwenye mpango huo.

Nchi nyingine za Afrika ambazo hazimo katika orodha ya upokeaji chanjo ni pamoja na Equatorial Guinea, Eritrea, Gabon, Lesotho, Madagascar na Ushelisheli.

WHO, linasema nchi ambazo hazimo katika orodha yake ya kupewa chanjo ya corona ni kwa sababu zilijinunulia chanjo zake zenyewe, na kwamba hazikuomba au hazikuwekwa katika orodha ya nchi zitakazopewa chanjo.

Miongoni mwa nchi za ukanda huo, zilizo kwenye orodha ya kupatiwa chanjo ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), itakayopata kiasi cha chanjo milioni 6.9, Kenya milioni 4.2, Rwanda milioni 1.1.

Nyingine zitakazopokea chanjo ni Sudan Kusini itakayopokea chanjo 864,000 huku Uganda ikitarajia kupokea chanjo 3.5.

WHO ilisema kuwa chanjo hizo ambazo ni dozi milioni 336 za AstraZeneca/Oxford na Pfizer-BioNTech, zitatolewa kwa muhula wa kwanza na wa pili kwa mwaka huu.

Nchi zitakazopewa ni sawa na asilimia 3.3 ya watu katika kila nchi katika mpango huo kulingana na malengo ya shirikisho la chanjo duniani (GAVI) kutoa chanjo kwa asilimia tatu ya wakazi duniani kipindi cha miezi sita ya kwanza mwaka huu.

***BBC***



Mfanyakazi wa Huduma ya Uvuvi ya Taifa (SERNAPESCA) nchini Chile, akiangalia samaki waliokufa na kuletwa na maji ya ufukweni eneo la Horcones, jana. **PICHA/REUTERS**

# Geterres ataka dunia kupinga mapinduzi Aung San akishtakiwa

**Naypyitaw, MYANMAR**

MAHAKAMA ya Myanmar, imemfungulia mashtaka kiongozi aliyepinduliwa, Aung San Suu Kyi, kwa tuhuma za kukiuka sheria kuhusu uagizaji na uuzaji bidhaa kimataifa.

Kwa mujibu wa Msemaji wa chama cha kiongozi huyo cha Umoja wa Kitaifa kwa Demokrasia (NLD), Kyi Toe.

Polisi nchini Myanmar iliwasilisha mashtaka dhidi ya Kyi kwa kumiliki redio kadhaa kwa mawasiliano ya nyumbani kwake, kinyume cha sheria.

Kwenye ukurasa wake rasmi wa Facebook, Kyi Toe aliandika kwamba, wamepata taarifa za kuaminika kwamba mahakama ya Dakhinathiri iliamuru San Suu Kyi kuwekwa rumande hadi Februari 15.

Alisema pia Rais Win Myint ambaye naye aliwekwa kizuizini kufuatia mapinduzi ya kijeshi yaliyofanyika siku ya Jumatatu, alishtakiwa chini ya sheria ya janga la kitaifa.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, alitoa wito wa kutekelezwa kwa katiba nchini Myanmar.

Alisema ana matumaini kwamba kutakuwa na umoja katika Baraza la Usalama la umoja huo, wakati wa kujadili suala hilo.

"Tutafanya kila tunaloweza kuleta pamoja washikadau muhimu katika jumuiya ya kimataifa kutoa shinikizo zaidi kwa Myanmar kuhakikisha kuwa mapinduzi hayo yanashindwa," alisema Guterres na kuongeza...

"Haikubaliki kabisa kubadilisha matokeo ya uchaguzi na matakwa ya wananchi."

Katibu huyo aitaka dunia kuhakikisha mapinduzi ya Myanmar yanashindwa.

Aidha, Wizara ya Mawasiliano na Habari, Myanmar, ilisema katika ukurasa wake mtandao wa Facebook kwamba, itazuiwa huduma za mtandao huo hadi Februari 7, mwaka huu.

Wizara ilisema lengo ni kuweka hali ya utulivu nchini humo, huku huduma nyingine ikiwamo Messenger, Instagram na WhatsApp zikizuiliwa pia.

***DW/BBC/VOA***

# Kundi la IS laua 19 katikati mwa Syria

**Hama, SYRIA**

WANAMGAMBO wa kundi linalojiita Dola la Kiislamu (IS), wamewaua maofisa 19 wa serikali ya Syria.

Pia wanamgambo kadhaa wanaounga mkono utawala huo, waliuawa katika tukio hilo lililotokea jana, katikati ya mkoa wa Hama.

Hayo ni kwa mujibu wa Shirika la Kutetea Haki za Binadamu, lenye makao yake nchini Uingereza.

Shirika hilo lilieleza kwamba miongoni mwa waliouawa kwenye shambulizi hilo la kundi la IS lililofanyika asubuhi, ni wapiganaji hao wa serikali na washirika wake wakiwamo wapiganaji 11 wa kundi la wanamgambo liitwalo Baqir Brigade, linaloungwa mkono na Iran.

Lilisema kuwa shambulizi hilo la kushtukiza la kundi la IS, lililenga vituo vya serikali Mashariki mwa Hama, eneo ambalo limekumbwa na makabiliano katika siku za hivi karibuni kati ya vikosi vya serikali na wanamgambo.

Kulingana na shirika hilo, zaidi ya watu 387,000 wameuawa Syria tangu vita vilipoanza nchini humo mwaka 2011.

***DW***

# Kiongozi wa waasi ahukumiwa ICC

**The Hague, UHOLANZI**

MAHAKAMA ya Kimataifa ya makosa ya Uhalifu wa Kivita (ICC), imemkuta na hatia mbabe wa zamani wa kivita wa kundi la Lord Resistance Army (LRA), Dominic Ongwen na kukutwa na makosa ya uhalifu dhidi ya binadamu.

Akisoma hukumu hiyo mjini The Hague, Jaji Bertram Schmitt, alisema hatia yake imepatikana bila ya shaka yoyote.

Hukumu iliyotolewa jana, inafuatia kesi ya zaidi ya miaka minne iliyoanza mwaka 2016, ikimtuhumu kiongozi huyo wa zamani wa waasi, kuwa na dhima katika uhalifu wa kutisha uliofanywa na kundi la LRA. Ongwen alikabiliwa na mashtaka 70 kwa matendo ya kikatili, yaliyofanywa mwanzoni mwa miaka ya 2,000 na kundi la waasi la LRA ambalo kiongozi wake, Joseph Kony alianzisha uasi mkubwa ukilenga kuunda taifa jipya chini ya misingi ya amri 10 za Mungu kama zilivyo kwenye Biblia.

Kesi dhidi ya Ongwen, ilijikita kwenye uhalifu uliotendwa baina ya mwaka 2002 hadi 2005, kipindi ambacho waendesha mashtaka walisema LRA, ilifanya mauaji, ubakaji, utumwa wa ngono, ndoa za kulazimisha, utesaji, uporaji na kuwasajili watoto chini ya umri wa miaka 15 kuwa wapiganaji.

Kesi hiyo ya kwanza mahakamani, ilmhusisha mtuhumiwa ambaye ni mwathiriwa wa uhalifu wa kivita uliofanywa na LRA, kwa sababu Ongwen mwenyewe alitekwa nyara na waasi akiwa mtoto alipokuwa njiani kuelekea shuleni.

Ongwen, aliyepachikwa jina la utani la siafu mweupe, pia ni mpiganaji wa kwanza wa kundi la LRA, kukabiliwa na mashtaka kwenye mahakama hiyo na kwengineko kuhusiana na madhila ya umwagaji damu, uliofanywa na kundi hilo katika mataifa manne ya Afrika.

Mbabe huyo wa kivita mwenyewe alijitetea na kuapa, hana hatia na mawakili wake walisema mara kadhaa kwamba, mashtaka dhidi yake sharti yaondolewe kwa sababu Ongwen aliathiriwa kisaikolojia kwa kuchukuliwa mateka na waasi alipokuwa mtoto.

***DW***




# DORTMUND

## KUMUUZA SANCHO BEI NAFUU

**DORTMUND, Ujerumani**

KLABU ya Dortmund imeripotiwa ipo tayari kumuuza, Jadon Sancho kwa pauni milioni 88 wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 alikuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Manchester United mwaka jana, lakini BVB walidaiwa hawakuwa tayari kushuka bei ya pauni milioni 108 ili kumuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa England.

Sancho amepata changamoto katika kuonyesha ubora wake katika kiwango ambacho alitarajiwa kwa Dortmund kipindi hiki, lakini bado ameweza kuchangia mabao nane na kutoa pasi za mwisho 13 katika mechi 25 kwenye mashindano yote.

Ripoti ya hivi karibuni imedai kwamba kuwasili kwa Amad Diallo kwenye Uwanja wa Old Trafford kunafanya Mashetani Wekundu kusitisha harakati za kumnasa Sancho, ambaye bado ana mkataba hadi mwaka 2023.

Hata hivyo, kwa mujibu wa gazeti la Bild, Dortmund wana nia ya kujaribu kuwashawishi United msimu huu wa majira ya joto, ili kupunguza bei yao hadi pauni milioni 88, ambayo inadhaniwa ni punguzo la pauni milioni 20.

Sancho, ambaye alikuwa akihusishwa na Chelsea na Liverpool, amefunga mabao 42 na kutoa asisti 56 katika

## RAMIRES ATAKA KUSTAAFIA AFRIKA KUSINI

**SAO PAULO, Brazil**

KIUNGO wa Chelsea na Ramires Santos do Nascimento anafikiria kucheza kwenye Ligi Kuu Afrika Kusini, wakati nyota huyo wa Brazil anafikiria huko ni sehemu sahihi ya kumaliza soka lake.

Ramires, ambaye ameitumikia Brazil mara 51, kwa sasa ni mchezaji huru baada ya kuichezea Palmeiras hadi mwisho wa mwaka jana.

Kwa mujibu wa gazeti la KickOff.com la Afrika Kusini, wakala wake wa Ureno, Simon Mimbire anafanya kazi kwa uhusiano na beki mstaafu wa Msumbiji, Helder 'Mano-Mano' Muianga juu ya uwezekano wa kuhamia kwenye ligi hiyo.

Ingawa kuna maslahi kutoka Qatar na Uturuki, PSL inabaki kuwa chaguo linalomvutia huku akiangalia ligi ambayo anaifuatilia na kulipa zaidi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 alitumia miaka mitano na nusu huko Stamford Bridge na kushinda Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi ya Europa, Ligi Kuu England, Kombe la FA na Kombe la Ligi.

Alishinda Kombe la Shirikisho la FIFA mwaka 2009 huko Afrika Kusini na akarudi mwaka uliofuata kwa Kombe la Dunia.

Ramires pia alicheza katika ushindi wa mabao 5-0 katika mechi ya kirafiki dhidi ya Bafana Bafana kwenye Uwanja wa FNB mnamo 2012.



## SARRI AKATAA KUINOA MARSEILLE

**MARSEILLE, Ufaransa**

MAURIZIO Sarri amekataa kuinoa Klabu ya Olympique Marseille baada ya kumsimamisha kazi, Andre-Villas Boas.

Jumanne, Marseille walimsimamisha kazi Villas Boas kutokana na kocha huyo kuweka wazi kutokubaliana na sera ya uendeshaji timu hiyo sambamba na kuandika barua ya kutaka kujiuzulu katika nafasi hiyo.

Uongozi wa Marseille uliamua kumsimamisha kazi mapema huku ikiweka taratibu za kinidhamu ambazo inaweza kmchukuliwa Villas Boas.

Katika kuhakikisha maisha yanaendelea, miamba hii ya soka la Ufaransa ipo sokoni kumsaka kocha atakayekinoa kikosi hicho kuelekea mwishoni mwa msimu.

Imeripotiwa kuwa Sarri alitajwa kama kocha anayewindwa na vigogo Marseille na akalikataa ombi hilo.

Sababu kuu ya Sarri kukataa kibarua hicho imetajwa kuwa, kocha huyo analenga kurejea kazini mwanzoni mwa msimu ujao sio katikati ya msimu huu.

Sambamba na Sarri, aliyekuwa kocha wa Borussia Dortmund, Lucien Favre, pia anahusishwa na Marseille wakati huu ambao mzunguko wa pili kwa msimu wa 2020/21 umepamba moto.

HABARI MICHEZO




# RUDIGER:

## SIJAHUSIKA KUTIMULIWA LAMPARD

**LONDON, England**

MLINZI wa Chelsea, Antonio Rudiger amekanusha kuhusika katika mazungumzo juu ya kutimuliwa kwa Kocha Frank Lampard.

Lampard alitimuliwa mwezi uliopita baada ya kushindwa kuirejesha timu kwenye kiwango kizuri na nafasi yake ikachukuliwa na Thomas Tuchel.

Na baada ya Tuchel kuchukua mikoba akamrejesha haraka Rudiger kuanza mara kwa mara kikosini.

Ripoti zinadai kwamba mlinzi huyo wa Ujerumani alikuwa ameitaka mamlaka huko Stamford Bridge kuchagua mabadiliko katika eneo hilo kwa sababu ya wakati wake mgumu chini ya Lampard, lakini amekanusha kutamka hivyo.

Akizungumza na The Athletic, Rudiger alisema: "Kumekuwa na uvumi mwingi wa upuuzi juu yangu kutoka wiki iliyopita. Sijawahi kuzungumza na bodi juu ya hali ya kocha au juu ya mada nyingine yoyote.

Lampard aliamini uwezo wangu baada ya Krismasi katika hali ngumu sana na nilishukuru kwa hii. Ilikuwa pia sababu kuu kwa nini niliwaambia wawakilishi wangu wasitafute uhamisho katika msimu wa baridi.

"Kwa bahati mbaya, haikukusudiwa kuwa kwa timu yetu itabadilisha mambo kwa kubadili kocha. Siku zote tulihitaji ustawi wa kocha na klabu.

"Alichukua nafasi ya ukocha msimu uliopita wakati mambo yakiwa magumu sana. Lakini tuliweza kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya pamoja.

"Amewapa nafasi wachezaji wengi wachanga katika kikosi cha kwanza na bado wanafanya kazi nzuri. Nina hakika tutamwona Frank Lampard akirudi tena katika klabu nyingine hivi karibuni."

Rudiger, ambaye alikuwa akihusishwa mara kwa mara na uhamisho msimu uliopita wa kiangazi, alianza mechi tatu za mwisho za Lampard za Ligi Kuu England.

# Hatima ya Messi yamvuruga Koeman

**BARCELONA, Hispania**

RONALD Koeman amekiri kwamba "hana imani" na Lionel Messi kama atabakia Barcelona zaidi ya msimu huu.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or ametumia muda wake wote wa kucheza soka pale Camp Nou, akichezea zaidi ya mechi 750 kwa miamba hao wa La Liga.

Messi alishindwa jaribio lake la kuondoka klabuni hapo msimu uliopita, lakini anamaliza mkataba katika muda wa miezi minne na anaweza kuanza mazungumzo na klabu nyingine kuhusu uhamisho kama mchezaji huru.


Barca ilikuwa na matumaini ya kumshawishi Messi akubali masharti mapya, ingawa Koeman bado hana uhakika kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina atabaki Katalunya.

"Sina imani na hilo," Koeman aliiambia The Athletic alipoulizwa ikiwa anafikiria Messi atasalia klabuni hapo.

"Nina matumaini, ndio, kwa sababu yeye bado ni mchezaji mzuri na bado anashinda mechi kwetu, kwa timu.

"Ninafurahia kuwa kocha wake. Ukiangalia sifa zake na uwezo wake kila siku kwenye mazoezi, ni jambo la kufurahisha. Kwa kweli, alikuja akiwa mtoto mdogo huko Barcelona. Na bado sioni Leo Messi akiwa kwenye jezi nyingine zaidi ya jezi Barca. "

Paris Saint-Germain na Manchester City wanachukuliwa kama mahali pekee ambapo Messi anaweza kwenda ikiwa ataondoka Barcelona majira ya joto.



# Van Dijk harudi dimbani msimu huu

**LIVERPOOL, England**

VIRGIL van Dijk hatacheza tena Liverpool msimu huu atahitaji "muujiza", hii ni kwa mujibu wa kocha, Jurgen Klopp.

Ilikuwa imeripotiwa kuwa Van Dijk angeweza kurudi Aprili, mwaka huu kutokana na jeraha la goti alilolipata Oktoba, mwaka jana.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 29 amekuwa akijiuguza huko Dubai na inasemekana alikuwa akikaribia kurudi uwanjani, lakini Klopp haoni kuwa hilo kama linawezekana kwa sasa.

"Chochote kinachotokea nadhani tuna nafasi ya Virgil kwenye orodha ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, nadhani alikuwa kwenye orodha ya Ligi Kuu England, hakuna mtu aliyeniambia lazima nibadilishe kitu. Ikiwa tuna nafasi katika orodha ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Virgil atakuwa kwenye orodha," aliuambia mkutano wa waandishi wa habari.

"Hakuna daktari aliyeniambia kuna nafasi ya Virgil kucheza tena msimu huu. Sitaki kusema haiwezekani, lakini haiwezekani.

"Ikiwa tuna nafasi tutawaweka wote hata wakati watu wa matibabu watawaambia hakuna nafasi kwa sababu tunaamini miujiza mara kwa mara.

Pamoja na Joe Gomez, Joel Matip na beki wa kati wa muda, Fabinho pia ameumia, Liverpool imemsajili Ben Davies kutoka Preston North End na Ozan Kabak kutoka Schalke siku ya mwisho ya usajili wa Januari.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MADRID, ALABA MAZUNGUMZO SAFI

Beki huyo wa Bayern anatarajiwa kuondoka Ujerumani baada ya kukubali kusaini mkataba...

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid wameripotiwa wamefikia makubaliano ya kusaini mkataba wa miaka minne na beki wa Bayern Munich, David Alaba.

Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 pale kwenye uwanja wa Allianz Arena unatarajiwa kumalizika ifikapo Juni mwishoni, mwaka huu.

Na klabu kadhaa zimeonyesha nia ya kuwania saini ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Austria.

Liverpool, Manchester United na Chelsea zote zilikuwa zinahusishwa na kumwinda beki huyo, lakini kwa mujibu wa Marca, Madrid wameshinda kwenye mbio hizo na wamefanikiwa kuinasa saini yake.

Ripoti hiyo inadai kwamba Alaba tayari amekubali kandarasi ya miaka minne na timu hiyo inayonolewa na Kocha, Zinedine Zidane, na hatua hiyo kuwa rasmi mara tu mkataba wake wa sasa na Bayern utakapomalizika msimu huo wa joto.

Beki huyo amekuwa mchezaji muhimu kwa klabu yake hiyo ya Ujerumani wakati wa msimu wa 2020-21, akichangia mabao mawili na kufanya usaidizi wa goli moja katika mechi 25 kwenye mashindano yote.

Alaba ameichezea Bayern Munich zaidi ya mechi 400 tangu mwaka 2010 alipojiunga nao kwa mara ya kwanza.

## KWA UFUPI

### TUCHEL AMTAJA UPAMECANO

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, ametoa kipaumbele kwa mlinzi wa RB Leipzig Mfaransa, Dayot Upamecano (22), na beki wa kati wa Bayern Munich raia wa Ujerumani, Niklas Sule mwenye miaka 25, kama wachezaji anaowalenga zaidi kuwasajili msimu huu. ***(Bild)***

### SANCHO BEI CHEE

KLABU ya Borussia Dortmund ipo tayari kupunguza dau lake kwa mchezaji wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20, kwa pauni milioni 20 na kubakia pauni milioni 88 kama njia moja ya kuchochea nia ya Manchester United kumsajili. ***(Bild, via Mirror)***

### WILDER KUULA ZAIDI

MMLIKI wa Sheffield United, Malkia Abdullah amesema ana ruhusa maalum kusafiri kutoka Saudi Arabia hadi England kumwarifu Kocha Chris Wilder kuwa kazi yake iko salama - hata kama klabu hiyo itashushwa daraja. ***(Talksport)***

### SHORETIRE KIMEELEWEKA

MANCHESTER United imefikiwa kuingia rasmi mkataba wa kwanza na winga, Shola Shoretire mwenye umri wa miaka 17, huku Paris St-Germain, Barcelona, Bayern Munich na Juventus zinamnyatia. ***(Mail)***

### BRAITHWAITE ALIGOMA

MSHAMBULIAJI wa Barcelona raia wa Denmark, Martin Braithwaite mwenye umri wa 29, alikataa matakwa ya West Bromwich Albion mnamo Januari na kuamua kubakia Nou Camp. ***(Sport)***

### LAMPARD, VIEIRA SOKONI

JOHN Terry na Patrick Vieira ni miongoni mwa makocha wanaowania kazi katika klabu ya Bournemouth baada ya Jason Tindall kufukuzwa. ***(Mail)***

### NIASSE ANUKIA HUDDERSFIELD

KLABU ya Huddersfield inafanya mazungumzo na mshambuliaji wa Senegal, Oumar Niasse, ambaye kwa sasa yuko huru baada ya kutoka Everton mwisho wa msimu uliopita. ***(Sun)***

### ANGELIN AGOMBEWA EPL

KLABU za Manchester United, Everton na Southampton zinafuatilia usajili wa mlinda mlango wa Celtic, Vincent Angelini mwenye umri wa miaka 17, ambaye mkataba wake wa sasa unaisha ifikapo mwisho wa msimu. ***(Tuttomercatoweb)***

### SARRI AKIKATAA MARSEILLE

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Chelsea, Frank Lampard na kocha wa zamani wa Juventus Maurizio Sarri wamekataa kuchukua nafasi ya kuinoa Marseille. ***(Sky Sports)***

### WILLOCK AJIONGEZA

KIUNGO wa Arsenal ambaye ni raia wa England, Joe Willock (21), amesema amefikia uamuzi wa kusaini kwa mkopo wa miezi sita katika klabu ya Newcastle kwa sababu alitofautiana na kocha Steve Bruce wakati anazungumza naye kwenye simu. ***(Chronicle)***

### BENZEMA NJIA PANDA

UAMUZI wa mshambuliaji wa Real Madrid, Karim Benzema kurejea Lyon kutategemea na matokeo ya upande wa klabu ya nchini Hispania. Raia huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 33, aliondoka Lyon na kujiunga na Real Madrid mwaka 2009. ***(Marca)***

HABARI MICHEZO

# BEKI TEGEMEO AZAM KUIKOSA SIMBA J'PILI

**Na Saada Akida**

BEKI wa Azam FC, Yakubu Mohammed ataukosa mchezo wa 'kiporo' wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya mabingwa watetezi, Simba kwa sababu ya kutumikia adhabu ya kadi tatu za njano alizopata katika mechi zilizopita za mzunguko wa kwanza, imeelezwa.

Simba inatarajia kuikaribisha Azam FC katika mchezo wake wa kiporo utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), beki huyo alionyeshwa kadi ya njano katika mchezo wa mzunguko wa 18 na kufikia idadi ya kadi tatu na hivyo hataruhusiwa kucheza mechi hiyo inayofuata.

Akizungumza na gazeti hili jijini, Kocha Mkuu wa Azam FC, George Lwandamina, alisema licha ya kumkosa nyota huyo hawataingia kwa presha kukabiliana na Simba kwa sababu wanaifahamu vyema.

Lwandamina alisema kazi kubwa ambayo anaifanya ni kuhakikisha anaimarisha kikosi chake na kutumia siku mbili zilizobakia kufanyia kazi mapungufu ya wachezaji wake ambayo aliyabaini katika michezo ya kirafiki waliyocheza hivi karibuni.

"Utakuwa mchezo mgumu, Simba ni timu nzuri na wameimarisha kikosi chao, hata sisi tumejipanga kwenda kutafuta pointi tatu muhimu, kwa upande wetu tunaendelea na maandalizi kwa ajili ya mechi hiyo," alisema Lwandamina.

Kocha huyo wa zamani wa Yanga alisema kikubwa wachezaji wake wanatakiwa kupambana, kujiamini na kujituma zaidi watakapokuwa uwanjani ili kuhakikisha makosa yaliyopita hayajirudii.

Alisema ameona udhaifu wa wachezaji wake wanapokuwa wanaongoza mchezo, na kutoa nafasi kwa wapinzani kusawazisha, hali iliyowatokea kwenye michezo miwili ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Namungo FC na Ruvu Shooting.

"Nimeona tena wamekuwa na tabia ya kuridhika wanapoona wako mbele hata tulipocheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya TP Mazembe (vigogo wa Jamhuri ya Kidemokrasia wa Congo- DRC), ninawakumbusha kuacha kujisahau," Lwandamina alisema.




Mshindi wa mechi 11 za Jackpot bonus, Maulidi Ngonyani, akishikilia mfano wa hundi ya Sh. milioni 7.5 aliyokabidhiwa na Kampuni ya SportPesa. Jackpot kwa wiki hii ni Sh. milioni 441.9 kwa atakayepatia mechi zote 13. Watakaobashiri kwa usahihi kuanzia mechi 10 hadi 12 pia watapata bonasi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# KMKM yawaza ubingwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LICHA ya kulazimishwa sare ya bila kufungana na Black Sailor, benchi la Ufundi la KMKM limesema bado inaamini ina nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu wa 2020/21.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema amefurahi kuona kikosi chake kimeanza vizuri katika mzunguko wa pili dalili ambayo inawaonyesha wanaweza kufikia malengo yao.

Msimu alisema wamejiandaa kupambana katika kila mchezo kwa sababu wanafahamu vizuri hatua ya lala salama huwa na ushindani zaidi.

"Tulianza mzunguko wa kwanza vizuri na tuliumalizika mzunguko huo tukiwa tunaongoza kwenye msimamo, ni matumaini yangu kama tulivyoanza vizuri mzunguko wa mwisho, tutamaliza hivyo hivyo," alisema Msimu.

Kocha huyo alisema mzunguko wa kwanza ligi hiyo ulikuwa mgumu kutokana na kila timu iliitaka kupata matokeo mazuri na kujiweka katika sehemu salama kwenye msimamo wa ligi kwa kuvuna pointi.

"Kilichopelekea ugumu wa ligi ni uchache wa timu zinazoshiriki, msimu huu tumekuwa na timu 12, kila timu haitaki kushuka daraja, kila upande unapambana kujilinda kubakia kwenye ligi hii huku baadhi wakiwa kwenye mbio za kuwania ubingwa, unaposhinda, ujue wachezaji wamefanya kazi kubwa ya ziada," alisema kocha huyo.

KMKM yenye pointi 20, imemaliza mzunguko wa kwanza ikiwa inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikifuatiwa na KVZ yenye pointi 20 huku Kipanga yenye alama 18 iko kwenye nafasi ya tatu.

## Mbeya City FC yatarajia mazuri

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mbeya City umesema maboresho waliyoyafanya kwenye kikosi na benchi la ufundi ya timu hiyo, wanaamini kikosi chao kitaendelea kubakia kwenye ushindani wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu mingine mbalimbali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Mbeya City, Emmanuel Kimbe, alisema wamejipanga kufanya vyema ili kujiepusha na janga la kushuka daraja.

Kimbe alisema maboresho waliyofanya ya kuajiri Kocha Mkuu mpya kutoka Uganda, Mathias Lule na kusajili wachezaji wengine katika kipindi cha dirisha dogo wamesaidia kukiimarisha kikosi chao.

Alisema baada ya kuingia makubaliano na Lule, wamewekа mikakati ya kupambana katika kila mechi watakazocheza ili kuvuna pointi na kujiondoa kwenye nafasi ya hatari.

"Timu imeingia kambini tangu Jumatatu ya Februari Mosi, hatuko katika nafasi nzuri kwenye msimamo, kabla ya kuingia kambini tulikutana na kocha wetu tukamweleza mipango ikiwa haina tofauti na mikakati yake, kikubwa anahitaji kuandaa timu na kutafuta pointi muhimu kila mechi," alisema Kimbe.

Aliongeza wanasubiri ratiba ya ligi ili kujua kikosi chao kitaanza wapi ingawa wakati tayari kucheza popote.

"Tuna imani ya kufanya vizuri, ukiangalia katika msimamo wa ligi, timu tumepishana pointi moja hadi mbili, ikiwamo Mwadui waliopo juu yetu wametuzidi pointi mmoja, tutapambana kufanya vizuri, tutapindua meza," alisema Kimbe.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Mbeya City yenye pointi 14 wako nafasi ya 17 wakati Ihefu FC ambayo pia ni ya jijini Mbeya yenye pointi 13 ndio inaburuza mkia.

Yanga yenye pointi 44 ndio vinara wa ligi hiyo ikifuatiwa na mabingwa watetezi Simba ambayo jana jioni ilikuwa ugenini ikicheza dhidi ya Dodoma Jiji na Azam FC yenye pointi 32 iko kwenye nafasi ya tatu.

Ligi Kuu Tanzania Bara ndiyo inayotoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati bingwa wa Kombe la FA hupata nafasi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Michezo
Ijumaa Februari 5, 2021
Nipashe



## MADRID, ALABA MAZUNGUMZO SAFI

HABARI UK 22



Winga wa Simba, Bernard Morrison (kulia), akijiandaa kumtoka mchezaji wa Dodoma Jiji FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana. Simba ilishinda 2 - 1. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA YALA KIPORO KWA NDIMU DODOMA

## ●●●Cha Namungo kimechacha, Morrison...

**Na Adam Fungamwango**

BAO la dakika ya sita baada ya saa ya mchezo, lililofungwa na kiungo mshambuliaji mtukutu Benard Morrison, liliifanya Simba kumkaribisha Kocha Mkuu, Didier Gomes Da Rosa, kwa ushindi wa 2-1 dhidi ya Dodoma Jiji kwenye Uwanja wa Jamhuri jana.

Ilikuwa mechi ya kwanza ya Ligi Kuu kwa kocha huyo, akipata ushindi ambao haukuwa rahisi kupata pointi zote za 'kiporo' hicho kilichokuwa hatarini kuchacha.

Ilikuwa ni kazi kubwa ya Rally Bwalya aliyempiga mtu kanzu katikati ya uwanja na kuukokota mpira kwa umbali mrefu kabla ya kumpasia mchezaji mpya, aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo akitokea FC Platinum, Perfect Chikwende aliyetoa pande kwa Morrison ambaye alipiga shuti lililompita kichwani kipa Aron Kalambo na kujaa wavuni.

Ilikuwa mechi ya kwanza pia kwa Chikwende Ligi Kuu, Mzimbabwe huyo akiingia kwenye rekodi ya kucheza mechi moja na kutoa pasi ya goli.

Hilo ni goli la pili kwa Morrison kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara tangu ajiunge na Simba, akitupia la kwanza Novemba 21 mwaka jana, kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, Simba iliposhinda 7-0 dhidi ya Coastal Union.

Simba ililazimika kusubiri hadi dakika ya 20 kufanya shambulizi kwenye lango la Dodoma Jiji, ilipopiga shuti la kwanza kupitia kwa Luis Miquissone na dakika tisa baadaye, ikapata bao la kwanza kupitia kwa straika wake hatari, Meddie Kagere aliyeunganishwa kwa kichwa krosi ya Morrison iliyotokana na kona fupi.

Hiyo ni mechi ya pili kwa Kagere kufunga kwenye uwanja huo msimu huu, akifanya hivyo kwenye mechi dhidi ya JKT Tanzania alipotupia mara mbili, Simba ikishinda mabao 4-0 Oktoba 4, mwaka jana.

Hata hivyo, goli la Mnyarwanda huyo la jana, lilidumu kwa dakika sita tu, Dodoma Jiji wakasawazisha kupitia mpira wa kona ambao mabeki wa Simba walishindwa kuruka na kumrahisishia Cleophace Mkandala kupiga kichwa kilichomwacha kipa Aishi Manula akijilaumu kwa uzembe wa safu yake ya ulinzi.

Kwa matokeo hayo, Simba imefikisha pointi 38 baada ya mechi 16, ikiwa ni pungufu kwa pointi sita kuwakamata vinara Yanga ambao wamecheza mechi mbili zaidi. Dodoma Jiji baada ya kipigo inabaki na pointi 22 kwenye nafasi ya 10 baada ya raundi 18.

Kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, KMC iliitandika bila huruma Namungo FC mabao 3-0 katika mechi nyingine ya kiporo cha Ligi Kuu.

Walikuwa ni wachezaji waliokuja kwenye kikosi hicho kipindi cha dirisha dogo, Charles Ilamfya aliyetoka Simba kwa mkopo na straika wa zamani wa Yanga, Mateo Antony, aliyesajiliwa kutoka KMKM ya Zanzibar, waliopachika bao kila mmoja, huku lingine likitokana na Namungo kujifunga wenyewe.

Kwa matokeo hayo, Namungo inashuka hadi nafasi ya 15 kwenye msimamo wa ligi hiyo ya timu 18, ikibaki na pointi zake 18, KMC ikipanda hadi nafasi ya sita, ikifikisha pointi 25.

## MASHABIKI YANGA WAMSUBIRI FISTON

**Na Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimebakia siku chache kuanza kwa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara, mshambuliaji mpya wa Yanga, Fiston Abdulrazack, anaonekana kuwa na deni kwa mashabiki wa timu hiyo ambayo bado hawana safu ya ushambuliaji yenye makali.

Raundi ya 19 ya Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kufanyika kuanzia Februari 13, mwaka huu, lakini kwa sasa mabingwa watetezi, Simba na Namungo zilizokuwa na majukumu ya kimataifa, zinaendelea kucheza mechi zao za 'viporo'.

Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, aliliambia gazeti hili lengo la kumsajili Fiston ni kuimarisha safu ya ushambuliaji ambayo aliikuta kwenye kikosi chake.

Kaze alisema anataka kuona timu yake inavuna pointi tatu katika kila mechi huku wakisindikizwa na idadi kubwa ya mabao.

Alisema katika kuhakikisha wanapata matokeo mazuri, amekuwa akifundisha mbinu mbalimbali za kufunga na kuzuia ili wafikie malengo ya klabu hiyo.

"Tutakuwa na kikosi imara ambacho hakijawahi kuonekana kwenye Ligi Kuu, tumedhamiria kuchukua makombe yote msimu huu, hiyo ndio mikakati tuliyonayo," Kaze ambaye tayari ameshinda Kombe la Mapinduzi mapema mwaka huu alisema.

Katika kuimarisha kikosi chake kuelekea hatua ya lala salama ya ligi hiyo, Yanga iliwasajili pia Dickson Job, Saidi Ntibazonkiza, huku pia ikiongeza nguvu kwenye benchi lake la ufundi kwa kumwajiri kiungo wake wa zamani, Nizar Khalfan kama Kocha Msaidizi na Mghana Edem Mortotsi ambaye ni kocha wa viungo.

Safu ya ushambuliaji wa Yanga inaongozwa na Michael Sarpong na beki, Lamine Moro ambao kila mmoja amefunga mabao manne.

Wakati huo huo, Yanga inatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya African Sport kutoka Tanga itakayofanyika kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002